

KUCHUNGUZA FASIHI YA MAJINA YA MITAA MJINI UNGUJA

HALIMA ALI HASSAN

TASNIFU IMEWASILISHWA IKIWA NI SHARTI PEKEE LA KUHITIMU

SHAHADA YA UZAMILI (M.A. KISWAHILI - FISIHI) YA CHUO KIKUU

HURIA CHA TANZANIA

2017

UTHIBITISHO

Aliyeta saina hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma kazi hii na anaidhinisha ikubaliwe kwa utahini na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania tasnifu yenye mada: **“Kuchunguza Fasihi ya Majina ya Mitaa Mjini Unguja”** na nimeridhika kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuwasilishwa kwa ajili ya Utahini wa Shahada ya Uzamili ya (M.A. Kiswahili - Fasihi) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....

Prof. Dkt. Sheikh T.S.Y.M Sengo

(Msimamizi)

.....

Tarehe

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga, kunakili. Kutarijumu, kuhifadhi au kutoa kivuli, japo sehemu ndogo ya tasnifu hii kwa njia yoyote ile na kwa mfumo wowote ule, bila idhini ya maandishi, kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa niaba yake.

TAMKO

Mimi, **Halima Ali Hassan**, ninakiri kwamba tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe, na kwamba kazi hii haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya shahada hii au tunzo yoyote.

.....
Saini

.....
Tarehe

TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa wanangu wapenzi Aisha, Ilham, Zainab, Faika, hairiyya na Zulekha kwa uvumilivu wao ulionifanya nikaweza kumaliza kazi hii kwa utulivu wa hali ya juu. Pamoja na mume wangu mpenzi bwana Abdalla Ibrahim na watoto wangu wa kulea Laylat, Shadida na Hadi. Aidha natabaruku hidaya hii kwa mama yangu mpenzi Mtumwa Suleiman kwa kunilea kwa mapenzi, busara na ushauri wake kila ninapopambana na vikwazo vya maisha huniongoza njia bora iliyonisaidia kufikia hatua hii ya kufanya utafiti huu kwa mafanikio makubwa.

SHUKURANI

- | | |
|--|--|
| 1. Kuanzia shukurani,
Zende kwa Mola Manani,
Yeye Hana mpinzani
Kapwekeka yu pekeya. | 6. Mola wetu Subhana,
Mpe maisha mapana,
Azidi kulea wana,
Sana twamhitajiya. |
| 2. Wa pili, mama mpenzi
Yeye ni wangu mzazi
Kanilea kwa mapenzi
Mengi amenifanziya. | 7. Mola Akupe thawabu,
Wewe ndiwe athbabu,
Uliyetoa majibu,
Hadi kazi kutimiya. |
| 3. Pia wangu la azizi,
Naye ni mume mpenzi
Kwa mahaba na mapenzi,
Kazi kunisaidiya | 8. Na wenzangu wanakozi,
Hawakuwa na mapozi,
Kubwa walifanya kazi,
Msaada kunipatiya. |
| 4. Katu sifanyi ajizi
Kumtaja mkufunzi,
Alonipa utambuzi,
Kazi kunismamiya. | 9. Chuo kikuu Huria
Siwezi kukiachia,
Kimetuonesha njia,
Elimu twajipatiya. |
| 5. Huyo ni professa Sengo,
Ambaye hana maringo,
Yeye kwetu sisi Hengo,
Mola katuzawadiya. | 10. Pia wanangu wapenzi,
Kwa huba niliwaenzi,
Kuwalea kwa malezi
Allah aliyoridhiya. |

11. Baada kutaja wana,
Kubwa kazi nilifanya,
Ya data kuzikusanya,
Utafiti kutimiya.

12. Kubwa kazi nilifanya,
Kwa usiku na mchana,
Data nilizikusanya,
Hadi kazi kutimiya.

13. Mada dhima ya majina,
Mola Ndiye Mwenye shina,
Alomfundisha sana,
Adamu wetu Nabiya.

14. Hiyo ndiyo nadharia,
Ambayo tulochukua,
Qurani yatwambia,
Hakuna lilibakiya.

15. Ni elimu ya msingi,
Katu sifanye ajizi,
Basi sote tuienzi,
Isije ikapoteya.

16. Mwisho ninamalizia,
Kutoa wangu wasia,
Katu msije wachia,
Elimu kujipambiya.

IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza fasihi ya majina ya mitaa ya Mjini Unguja. Ndani ya majina ya mitaa mna siri nyingi zilizojificha zinazohitaji uweledi ili kuweza kuzifumbua. Mtafiti amechunguza fasihi ya majina ya mitaa kwa kubainisha fani iliyounda majina hayo kwa kuchambua kipengele cha mtindo na lugha ya kifasihi iliyotumika. Vilevile, alichambua maudhui kwa kubainisha asili ya majina ya mitaa na ujumbe, kwa kuongozwa na nadharia ya uhalisia na nadharia ya ndani nje. Utafiti umefanyika katika maeneo ya Mjini Unguja ndiko watafitiwa walikosailiwa. Jambo la kufurahisha na la kutia moyo ni ushiriki wa viongozi wa juu wa Serikali na wazee mashuhuri, katika kutoa data zilizofanikisha utafiti huu. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa majina ya mitaa yanachambulika kifasihi. Kwa Ujumla, utafiti uliongozwa na madhumuni matatu ambayo yalisaidia kubainisha fasihi ya majina ya mitaa iliyopo Mjini Unguja. Madhumuni ya kwanza kuchambua asili ya majina ya mitaa matokeo yameonesha kuwa majina hayo yameanza kwa sababu maalumu ya kihistoria na kimazingira. Madhumuni ya pili kuchunguza vipengele vya fani ambavyo ni lugha na mtindo. Matokeo yanaonesha kuwa, majina ya mitaa yameundwa kutokana na kaida maalum kama vile, mbinu ya umashuhuri, mbinu ya mazingira na usababishi. Majina ya mitaa yameundwa kwa kutumia lugha ya kifasihi yenye mvuto, inayotoa taswira kwa jamii yenye tamathali za semi kama vile tash biha, tauria, tash hisi, mafumbo na tanakali sauti. Madhumuni ya tatu kueleza ujumbe unaopatikana katika majina ya mitaa Mjini Unguja. Matokeo yameonesha kuwa majina yanatoa ujumbe wa jumla kama vile kulinda utamaduni, utambulishi na kuhifadhi historia.

YALIYOMO

UTHIBITISHO	ii
HAKIMILIKI	iii
TAMKO	iv
TABARUKU	v
SHUKURANI.....	vi
IKISIRI	viii
ORODHA YA MAJEDWELI	xiii
ORODHA YA VIAMBATANISHI	xiv
ORODHA YA VIFUPISHI.....	xv
SURA YA KWANZA.....	1
UTANGULIZI WA JUMLA	1
1.1 Usuli wa Mada	1
1.2 Tatizo la Utafiti	3
1.3 Lengo la Utafiti	4
1.4 Madhumuni Maalumu	4
1.5 Maswali ya Utafiti	5
1.6 Umuhimu wa Utafiti.....	5
1.7 Hitimishi	5
SURA YA PILI	7
UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA	7
2.1 Utangulizi.....	7

2.1.1	Utalii wa Kazi Tangulizi.....	7
2.1.2	Asili ya Majina.....	7
2.1.2	Asili ya Koo.....	16
2.1.3	Majina ya Semi.....	19
2.1.4	Hitimishi.....	21
2.2	Uhakiki wa Nadharia.....	21
2.2.1	Nadharia ya Uhalisia.....	21
2.2.3	Hitimishi.....	24
	SURA YA TATU.....	25
	MBINU ZA UTAFITI.....	25
3.1	Utangulizi.....	25
3.2	Mbinu za Kukusanyia Data.....	25
3.2.1	Mbinu ya Usaili.....	25
3.2.2	Mbinu ya Hojaji.....	26
3.3	Eneo la Utafiti.....	27
3.4	Mipaka ya Utafiti.....	29
3.5	Uteuzi wa Watafitiwa.....	29
3.6	Njia ya Uchambuzi wa Data.....	31
3.7	Hitimishi.....	31
	SURA YA NNE.....	32
	UCHAMBUZI WA DATA.....	32
4.1	Utangulizi.....	32
4.2	Asili ya Majina ya Mitaa.....	32
4.2.1	Majina Yenye Asili ya Miti.....	32

4.2.1.1 Majina Yanayotokana na Miti	33
4.2.1.2 Mwembe	33
4.2.1.3 Mitaa Inayotokana na Mbuyu	39
4.2.1.4 Miti Mingineyo	40
4.2.2 Majina Yenye Asili ya Watu	43
4.2.2.1 Majina yenye Asili ya Watu	44
4.2.3 Majina Yaliyotokana na Mazingira.....	47
4.2.3.1 Majina ya Mazingira.....	47
4.2.4 Majina ya Matukio	49
4.2.4.1 Majina ya Matukio	50
4.3 Kuchambua Vipengele vya Mtindo na Lugha	58
4.3.1 Mtindo.....	59
4.3.1.1 Mbinu ya Mwambatano.....	59
4.3.1.2 Mbinu ya Umashuhuri (Eponimu)	60
4.3.1.3 Mbinu ya Kimazingira (Toponimu)	60
4.3.1.4 Mbinu ya Usababishi na Tukio	61
4.3.2 Lugha	62
4.3.2.1 Tamathali za Semi.....	62
4.4 Ujumbe wa Majina ya Mitaa.....	67
4.4.1 Utamaduni.....	67
4.4.2 Utambulishi.....	68
4.4.3 Kuhifadhi Mapisi.....	69
4.5 Hitimishi	70

SURA YA TANO	71
MUHTASARI, HITIMISHI NA MAPENDEKEZO	71
5.1 Utangulizi.....	71
5.2 Muhtasari	71
5.3 Matokeo ya Utafiti.....	73
5.3 Mapendekezo	75
MAREJELEO.....	77
VIAMBATANISHI.....	85

ORODHA YA MAJEDWELI

Jedwali Na 3.1: Idadi ya Watu wa Mkoa wa Mjini	28
Jedwali Na 3.2: Uteuzi wa Watafitiwa.....	30
Jedwali Na 4.1: Majina ya Miti	33
Jedwali Na 4.2: Majina Yenye Asili ya Watu	44
Jedwali Na 4.3: Majina ya Mazingira	47
Jedwali Na 4.4: Majina ya Matukio.....	50
Jedwali Na 4.5: Mbinu ya Mwambatano	59
Jedwali Na 4.6: Mbinu ya Umashuhuri (Eponimu).....	60
Jedwali Na 4.7: Mbinu ya Kimazingira (Toponimu).....	61
Jedwali Na 4.8: Mbinu ya Usababishi na Tukio.....	61
Jedwali Na 4.9: Ujumbe wa Majina ya Mitaa	69

ORODHA YA VIAMBATANISHI

Kiambatanishi Na. I: Maswali ya Usaili kwa Wazee	85
Kiambatanishi Na. II: Maswali ya Hojaji kwa Viongozi.....	88
Kiambatanishi Na. III: Majina ya Mitaa	91

ORODHA YA VIFUPISHI

BAKIZA	Baraza la Kiswahili la Zanzibar
Bi	Bibi
Bw.	Bwana
SAMIKISA	Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu
SUZA	State University of Zanzibar
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
TATAKI	Taasisi ya Taaluma za Kiwashili
Z.B.C	Zanzibar Broadcast Cooperation
MM	Mwanamme
MK	Mwanamke

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Usuli wa Mada

Katika mapisi ya jamii za ulimwenguni, baada ya mwanadamu kupambana na hali ngumu ya mazingira yake, alijaribu kurahisisha maisha yake kwa kutumia fasihi ambayo ni sanaa tata ya maneno teule, inayoshughulikia masuala ya binaadamu matatizo yake, ndoto zake, migogoro yake, hisia na matamania yake, ili kujiletea maendeleo Wamitila (2006) watu wa Unguja hutumia fasihi ya majina katika maisha yao iliyokusanya mila, silka na utamaduni ili kukuza na kuendeleza utambulishi wao.

Majina yana kazi kubwa katika maisha ya kijamii. Ikichunguzwa kwa makini, majina hubeba maana, ambazo kimsingi, hueleweka na wanajamii wenyewe kwa sababu ni watu wenye maarifa, elimu na uzoefu wa maisha. Waandishi wa kazi za kifasihi huyatumia majina ya wahusika ambayo yanaakisi wasifu, tabia na itikadi zao (Wamitila, 2006), uteuzi wa majina ya wahusika unaweza kujitokeza kwa kuzingatia tabia zao katika matendo, maneno na mwelekeo wa nnje (Kennan, 2007), Abeid (2005), Majina ya mitaa yanaakisi hali halisi ya wenyeji. Ametoa mfano mtaa wa Jang'ombe unajulikana kwa vituko vyake, unapopita mitaa hiyo lazima uwe imara, amelinganisha jina la Jang'ombe na tabia za wenyeji kwa kusema 'ja' ni sawa na neno kama, hivyo watu wake wana tabia kama za ngombe. Aliusifu mtaa wa Mwera regeza mwendo ambako ni makazi ya mwanzo ya watawala wa kiarabu, ukipita hapo ukiambiwa na askari regeza mwendo ili usifanye fujo za viatu. Hivyo, majina hutoa ishara fulani kwa jamii husika.

Dhana ya majina si ngeni kwa wanajamii, mapisi yanatuelezea kuwa baada ya kuumbwa binadamu, alifundishwa majina ya vitu vyote, ili aweze kuyakabili mazingira yake (AlFarsi, 1993). Majina aliyofundishwa mwanaadamu ni ya vitu vyenye uhai na visivyo uhai atakavyo vitumia ulimwenguni katika maisha yake ya kila siku. Fasili ya majina imeelezwa katika mitazamo tafauti. Khamis (2011), Saluhaya (2010), Kihore na wanzake (2008), wameeleza jina ni aina ya neno linalotaja au kubainisha viumbe hai, vitu visivyo uhai, mahali, hisia, hali, maarifa au tukio katika tungo. Ally na wenzake (1930), wamefafanua kuwa, jina ni kila tamko analoitiwa mwanadamu, mnyama, mmea vitu vigumu (jamadu) au kitu kingine chochote.

Hivyo, majina ni maneno yanayotaja vitu, viumbe au hali ili kuviainisha na kuvitafautisha na vitu vyengine. Yapo majina ya kawaida kama vile, meza, nyumba, miti, na jabali. Yapo majina ya pekee ambayo huwa na umbo au tabia ya kipekee au ni kitu kimoja tu, ulimwenguni. Majina ya watu kama vile Kazija, John na Ali. Majina ya mahali kama Manzese, Kariakoo na Jang'ombe. Ni dhahiri kuwa duniani wapo Kazija wengi lakini kila Kazija mmoja ni tafauti na mwingine kiumbo na kitabia. Halikadhalika, Dar es Salaam, Unguja na Mombasa ziko sehemu ziiwazo Kariakoo lakini, kila Kariakoo moja ni tafauti kimaumbile na kimazingira na hizo nyengine.

Majina ya mitaa ni aina ya majina ya pekee, yanayopatikana ndani ya mji. Mfano, Mjini Unguja ipo mitaa kama vile, Rahaleo, Mkunazini na Jang'ombe. Kila mtaa huwa una chanzo chake, aghalabu ni tukio lililosababisha kuitwa hivyo, jina haliwezi kuitwa bila ya kuwepo historia ya kuitwa kwake. Mutembei (2009:31), anauliza

kwanini watu hutoa majina ya vitu, mahali, watu au matukio? Je! Jina ni jina tu au lina maana ndani yake? Je! Ni utambulishi au kielezeo cha yaliyopita au ni utabiri wa yatakayotokea? Akajibu maswali hayo Mutembezi (ameshatajwa), kwa kueleza kuwa, kwa vyovyote vile kuna msukumo unaowafanya watu watoe majina. Ama kwa hakika majina tunayopewa, huwa ni utambulishi wa asili zetu, kwa kumtambulisha mtu eneo analotokea, tabia na sifa zake na humtafautisha mtu mmoja na mwingine na hutolewa majina kwa kuzingatia fasihi ya sehemu inayohusika.

Majina ni kipengele kimojawapo cha fasihi chenye manufaa makubwa kwa jamii ya Ki-Unguja. Hutambulisha utamaduni wao, huwajaza asili na siri nyengine zilizomo ndani ya majina. Kutokana na maelezo hayo, inadhihirika kuwa. Majina ya mitaa, ni moja ya majina ambayo, huwa na chanzo, na hutoa ujumbe maalumu kwa jamii. Na ndiyo maana mtafiti amechagua mada hii ili aweze kuchunguza asili, lugha, mtindo na ujumbe unaopatikana katika majina ya mitaa ya Mjini Unguja.

1.2 Tatizo la Utafiti

Kwa kawaida, kila kitu kina jina ili kuweza kutafautishwa na kingine. Watu husema kuwa, majina huwa na sababu au chanzo. Majina ya mwezi, siku, majina ya watu na hata majina ya mitaa huwa na sababu na chanzo chake, huwa na dhima na hutoa ujumbe maalumu kwa jamii.

Kuna upotevu mkubwa wa mapisi ya majina ya mitaa kwani watu wengi hawafahamu chanzo chake na hapana sehemu zilikoandikwa, na wazee wengi waliokuwa wakifahamu wameshapoteza kumbukumbu kutokana na umri mrefu na wengine wameshafariki. Hali hiyo, imezusha, majina mapya mengi bila ya

mpangilio, yasiyoandamana na utamaduni wa Waswahili. Kuna majina kama vile, Toronto, Cossovo, Sarayevo katika mitaa ya Waswahili. Majina hayo si mageni tu kwa Zanzibar, lakini yanaharibu silka na hadhi na taadhima ya Mji wa Unguja. Suala hili limemshawishi mtafiti kujiuliza maswali mengi.

Je! Majina ya mitaa yana chanzo chake? Je! Wanajamii wanafahamu sababu za kuitwa hivyo? Je! Kuna uchambuzi wa kifasihi katika majina hayo? Majina ya mitaa ni utambulishi wa pahala husika. Muhimu kwa mtu binafsi, jamii hata Taifa la kila nchi hujulikana kwa jina. Mtu hutakiwa ajieleze wapi anaishi. Taifa nalo hujipangia mipango ya maendeleo kulingana na mahitaji muhimu ya mitaa.

Kutokana na umuhimu wa majina ya mitaa, mtafiti ametafiti namna ya kufumba na kufumbua. Maisha ni tata lakini watu wengi hawajui huo utata, wala hawajali kuwapo kwake. Jina ni kama uwa lililofumbwa, lenye mambo mengi, ndani yake. Hivyo, kitendawili cha majina, kimefanya mtafiti kuchunguza fasihi ya majina ya mitaa ya Mjini Unguja.

1.3 Lengo la Utafiti

Kuchunguza fasihi ya majina ya mitaa ya Mjini Unguja.

1.4 Madhumuni Maalumu

- (i) Kuchambua asili ya majina ya mitaa ya Mjini Unguja
- (ii) Kuchambua kipengele cha mtindo na lugha vinavyojitokeza katika majina ya mitaa ya Mjini Unguja.
- (iii) Kueleza ujumbe unaopatikana katika majina ya mitaa ya Mjini Unguja.

1.5 Maswali ya Utafiti

- (i) Ipi asili ya majina ya mitaa ya Mjini Unguja?
- (ii) Vipi kipengele cha mtindo na lugha vimejitokeza katika majina ya mitaa ya mjini Unguja?
- (iii) Majina ya mitaa ya Mjini Unguja yanatoa ujumbe gani?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utasaidia kupata taarifa ngeni. Majina yatafahamika zaidi kwa kutoa mapisi ya majina, na kugundua siri zilizojificha. Kama Waswahili wasemavyo. 'Usilolijua usiku wa kiza' (Ndalu 2008), Walimu na wanafunzi wataelewa fasihi iliyomo ndani ya majina ya mitaa kwa kugundua miundo iliyotumika, lugha, asili na ujumbe unaopatikana katika majina hayo. Wanajamii na hasa mamlaka za miji zitachukua hadhari katika kuteua majina ya mitaa, kwani, jina ndilo linalotoa picha halisi ya eneo. Serikali itanufaika kwa utafiti huu, kwani haitakiwi kubadilisha majina ya mitaa kiholela, kila mtaa una mapisi yake yaliyofungamana na fasihi ya sehemu hiyo. Hivyo, si vyema, kuwavurugia wenyeji majina yao yasiyolingana na fasihi yao. Mambo mengine, na hili mojawapo, hayataki siasa za kujipanua, kweli zibakie kweli za kihistoria.

1.7 Hitimishi

Utafiti huu wa Kuchunguza fasihi ya majina ya mitaa ya Mjini Unguja, ni utafiti wa sanaajadii ya. Kazi za sanaajadii ya, zimejikita katika mzunguko mzima wa maisha ya mwanadamu. Mapisi yanatuonesha kuwa, dhanna ya majina imeanza tangu mwanzoni mwa maisha ya mwanadamu. Majina huwa na asili ya kuitwa kwake,

huweza kuwa ya kimazingira au kimatukio. Aghlabu, majina hutoa maana maalumu inayofahamika na wanajamii. Utafiti huu unatarajia kuwa jicho la wanajamii, wanataalimu na watawala kulinda na kuhifadhi majina ya asili ili kudumisha mapisi na utamaduni wetu.

SURA YA PILI

UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Mtafiti ametalii machapishi kama vile, majarida, vitabu, wavupepe, tasnifu za kazi zilizotangulia na kusikiliza vyombo vya habari, zilizomsaidia mtafiti kupata data anazozihitaji kulingana na mada na madhumuni yake ya utafiti. Pons (1992), amefafanua utalii wa kazi tangulizi huhusisha kusoma nyaraka, machapisho yaliyoandikwa ambayo mtafiti anategemea kupata taarifa anazotafuta kulingana na mada na malengo yake ya utafiti. Pia, mtafiti amefafanua kiunzi cha nadharia zilizoongoza utafiti huu.

2.1.1 Utalii wa Kazi Tangulizi

Mtafiti amezigawa kazi tangulizi katika sehemu tatu ili kuweza kuipanga kazi yake kwa mtiririko mzuri na kupata urahisi wa kusoma na kuandika. Oliver (2004) Kuzipanga kazi tangulizi katika sehemu, zitakuwa nyepesi kuzisoma na kuziandika.

2.1.2 Asili ya Majina

Buberwa (2010), alifanya utafiti juu ya utoaji wa majina ya mitaa, aliyagawa majina katika makundi. Yapo yaliyotokana na majina ya miti, kama vile, mtaa wa Mishasha jina hili linatokana na mti uitwao mish-mish. Kisheka, linatokana na mti wa msheeka. Yapo majina yanayotokana na watu mashuhuri, matukio muhimu na imani za wanajamii, kama vile, Kikoromea, linatokana na sehemu ambayo watu wanajiandaa kwa ajili ya safari ya kwenda vitani. Rahaya, linatokana na itikadi na imani za wenyeji. Kahyoro, ni sehemu inayotumika kutilia makali silaha za kivita na

Ikondo ni sehemu inayopita maji. Utafiti huo umetoa mwangaza kwa mtafiti kugundua kuwa, majina hutolewa kwa sababu maalumu za kiitikadi au kimatendo.

Kihore na Chuwa (1999), wamechunguza mbinu za kubuni majina ya kibiashara. Wameona kuwa, kuna mbinu nyingi zinazotumika katika kutoa majina. Miongoni mwa mbinu hizo ni Mbinu ya kisitari, kwa kufananisha kazi au dhima. Mfano, dawa ya kuulia wadudu waharibifu huitwa komesha, kiboko na hongera. Kufananisha nguvu, uimara na uwezo. Mfano, saruji chapa mbuni, majani ya chai chapa simba. Majina ya kujiografia. Mfano, kibiriti chapa KIBO. Kiwanda cha vibiriti vya aina hii kipo Moshi eneo lililo karibu na kilele cha kibo cha mlima Kilimanjaro. Kazi hii imemuongoza mtafiti kugundua kuwa majina huwa na asili au sababu.

Haji (2014) alichunguza mifumo ya utoaji majina ya mitaa. Aliyagawa majina yanayotokana na mimea, Mkadini na Mwembemmoja. Majina ya matukio, Pagali, eneo hilo lilikuwa soko la bidhaa wakiwamo wanyama, kama vile paa, ambao ni kitoweleo waliuzwa kwa bei ya juu, hivyo wenyeji wakisema paa ghali. Kwa vile sauti'gh' ni ngumu kwao kuitamka walisema paagali ndilo lilipopatikana jina la Pagali. Mtaa wa Kidutani unatokana na maumbile ya eneo hilo ni sehemu iliyoinuka na nyumba zake ziko juu ya kilima sehemu yenye mawe mengi. Hanyegwa mchana, watu wa hapo walikuwa hawana vyoo katika nyumba zao, hivyo watu walifanya haja kubwa mwituni wakati wa mchana ndiyo sababu ya kuitwa Hanyegwa mchana ili kutoa tahadhari kwa wanajamii kuepuka kufanya haja ovyo, jambo ambalo liliwafanya watu kuanza kujenga vyoo majumbani. Kazi hiyo imemsaidia sana mtafiti kugundua kuwa majina ya mitaa pia ni sehemu ya fasihi kwani hutoa ujumbe kama zilivyo tanzu nyengine za fasihi.

Buberwa (2010), alichunguza Muundo wa majina ya mahali katika vituo vya daladala kwa kuelezea miundo iliyotumika katika kuunda majina ya vituo kama inavyooneshwa katika jadweli.

Jedwali Na 2.1: Mbinu ya Kuhamisha Maana

Jina la Kituo	Kituo kinapopatikana	Kichocheo
Mchicha	Barabara ya Changombe	Mchicha unalimwa karibu na sehemu hiyo
Biashara	Barabara ya Mandela	Kuwapo kwa Chuo cha Biashara

Chanzo: Utafiti (2015)

Jedwali Na 2.2: Mbinu ya Kijiografia (Toponimu)

Jina la kituo	Kituo kinapopatikana	Kichocheo
Darajani	Barabara ya Morogoro	Kuwapo kwa Daraja
Bondeni	Barabara ya chuo Kikuu	Kuwepo kwa Bonde

Chanzo: Utafiti (2015)

Hii ni mbinu ya kuunda majina kutokana na hali ya kijiografia ya eneo husika. Kazi hiyo imesaidia mtafiti kuchambua mitindo inayotumika ya kuundia majina ya mitaa. Amiri (2011), Msanjila na wenzake (2009), wamezungumzia umuhimu wa majina katika suala la utambulishi. Majina ya vitu na matukio muhimu, hutolewa kwa lugha inayozungumzwa na jamii na hubeba maana ambazo, kimsingi, zinaeleweka na wanajamii. Wametoa mfano wa majina ya watu na matukio. Kama vile, jina la ChonyaMagulu, linatokana na tukio la njaa lililotokea mwaka (1880), ambalo lililodhoofisha miguu na watu wengi kushindwa kutembea. Manzale, ni jina la mtoto aliyezaliwa wakati wa njaa. Matonya, amezaliwa wakati wa mvua. Pia,

Amiri (ameshatajwa) ameelezea majina yanayofungamana na lugha ya Kiswahili yanayokubalika kutumika katika utambulishi wa Mtanzania. Kama vile, majina ya familia; Mwinyi, Sokoine, Warioba. Majina ya matukio; Azimio la Arusha, Uhuru wa Tanganyika. Majina ya vivutio vya utalii; Mlima Kilimanjaro, Mto Kagera na Serengeti. Kutokana na maelezo hayo, mtafiti amepata kuelewa kwamba dhima kuu ya majina ni utambulishi.

Tabia (2011) amemnuuu Mwaruka (1965:70) anaeleza namna mtoto, anavyorithishwa jina la baba yake katika jamii ya Wazaramu. Mtani husimama sehemu ya katikati ya jeneza akiwa, na vijana wawili ambao ni vijana wa marehemu na kusema ‘mzee wenu leo amefariki na tangu leo namrithisha huyu mwanawe mkubwa jina la Mlawatangwi yaani mrithi wa baba, na yule mdogo ataitwa Mwenegoha, yaani naibu wake. Hivi ndivyo, wanavyorithishana majina, ingawa wengine hurithishwa majina mara tu baada ya kuzaliwa.

Denice (2011), Alhidaaya (2015), Strictly (2010), wameleza, majina mengi ya watu na mahali, yana maana. Mara nyingi maana hizo ni za kidini. Majina yanayotolewa, huonesha mawazo na tajriba za kidini. Kwa mfano, Nigeria, jina la Babatunde, ina maana ya baba karejea; hutolewa baada ya kuzawa mtoto wa kiume, Mariyamu, lenye maana ya mtumishi wa Mungu. Najiihi, aliyefaulu. Abraham, baba wa Mitume. Kwa kuifahamu fasihi ya majina. Sengo (2014 kutoka darasani), amesimulia alipawa jina la urithi wa babu yake mzaa mama, Tigiti, baada ya mama yake kwenda kutafiti kwanini mtoto wake kavunjwa mkono wa kulia shuleni. Hivyo, majina yanayotolewa huwa na maana na vyanzo vyake.

Abubakar (1998), ameelezea historia ya Zanzibar, wakati wa utawala wa kisultani walianzisha majengo. Kama vile, Beit-el Ajaib, iliyojengwa kwa nguzo za chuma na roshani zenye kuzunguka pembe nne, pambo lake ndani ni maandishi ya Qur-an, yaliyonakishiwa kwa wino wa dhahabu. Kutokana na namna lilivyojengwa, lilipawa jina la ‘Beit el Ajab’, lenye maana nyumba ya ajabu. Mtaa wa Mtoni, ulipewa jina hilo, kwa sababu jengo kongwe la Sultani wa Zanzibar lilikuwapo pembezoni mwa mto mdogo, uliotokea upande wa ndani wa kisiwa cha Unguja, uliopitisha maji yake masafa mafupi, baada ya kulipita jumba hilo, kuelekea pwani. Mtaa wa Chuini, kulikuwa na jumba kubwa lenye bustani kubwa iliyokuwa ikifugwa wanyama kina Chui, Simba na wengineo. Kutokanan na uasili wa majina ya Mitaa kazi hii itasaidia katika uchambuzi huu.

Chum (1982), ameeleza asili ya mitaa ya Mkoa wa Kusini Unguja. Paje, asili yake, mnyama aitwae paa, pamoja na kilimo cha choroko. Wenyeji walilima choroko, zilizitawi sana, lakini walikuwapo wanyama waitwao paa walikuwa wakizila sana. Hivyo, wenyeji wakawa wanasema choroko zimestawi sana lakini paajee? maana hawana njia ya kuwazuia wasizile. Kijini, pahala penye ardhi nzuri ya kilimo, wenyeji walivutika na sehemu hiyo. Walisema sehemu nyingi tumepita lakini hapa kiini hasa cha ardhi nzuri. Walilitumia neno kiini mara kwa mara lakini baadaye kutokana na hitilafu ya mapokezi kizazi hadi kizazi jina liligeuka na kuitwa Kijini. Hivyo tunaona kuwa kila jina la mtaa lina asili yake

Ingram (2007), Haji (2013), wameelezea asili ya neno Zanzibar, ‘Zinjiba’ linalotokana na lugha ya kifarsi, lenye maana ya ardhi nzuri ya watu wa pwani. Neno Unguja lina asili ya Kiswahili linatokana na neno Ungu-jaa lenye maana ya kisiwa

kikubwa chenye watu wengi, vyakula tele na ibada nyingi. Kwa upande wa kisiwa cha Pemba, asili ni neno la Kiswahili, ‘kupemba’ lenye maana ya kuongoza chombo kwa uangalifu kutokana na kuwa kisiwa hiki kimezungukwa na mkondo mkubwa wa bahari. Khamis na Omar (1993), wameeleza Unguja ndilo jina la asili. Wasafiri wamelitaja jina hilo, tangu karne ya (9A.D). Jina la Unguja Ukuu linatokana na umuhimu wa eneo hilo hapo zamani. Kazi hii imesaidia kujua uasili wa Majina ya Mitaa.

Jumuiya ya Demokrasia na Ushirikishaji (2007), wameelezea asili ya Unguja, walikuja wakaazi wa Bara, wakawakuta wenyeji wa Visiwani wakarimu sana waliwakaribisha vizuri na kuwapa vyakula na zawadi za kuchukuwa kwao. Walipofika Bara waliulizwa na wenzao “Huko Kisiwani kuna nini?” Walijibu “Vitu vingi ungo ujaa” yaani ungo uliojaa, unaoonesha utajiri na neema zilizokuwapo wakati huwo. Uzini, kulikuwapo wazee walioamua kuulinda Mji wao, walichimba mtaro, chini ya mtaro waliweka uzi uliofanyiwa dawa za matambiko, uliozungushwa kijiji chote, Watu walikuwa wanasema “Tunakwenda Uzini,” hapo ndipo lilipoanzia jina la Uzini. Mchango mkubwa umepatikana katika kuendeleza uchambuzi wa Majina ya Mitaa

Juma (2011), Haji na Rai (2009), wameeleza chimbuko la Wamakunduchi, lilitokana na kundi la watu lilofikia Unguja Ukuu, baadhi yao waliondoka na kuelekea kusini mashariki ya kisiwa, wakafika sehemu yenye udongo mwekundu, walisita hapo na kuanza shughuli za kilimo, baadaye, walirejea Unguja Ukuu. Walipofika, waliulizwa wanakotokea, wakajibu, ‘Tuwa uko nyikunduchi’ yaani sehemu yenye ardhi nyekundu. Rai na Haji (wameshatajwa) wameeleza asili ya Wamakunduchi,

walitokea Bagamoyo, pwani ya Tanganyika, juu ya Dar es Salaam, poti ndogo ya Kunduchi. Masoud (2005), ameeleza asili ya Makunduchi: kuwa, watu wa Makunduchi walikwenda kutembea Mtende, wakawaona wenyeji wa huko wamelima mazao mengi, wakasema ‘Ama nyie mtende. Maana nyinyi mmefanya kazi kubwa ya kilimo nao, wakajibu “kwani nyie mjikalii makunduuchi. Maana mumekaa bila ya kufanya kazi yeyote. Na hii ndiyo, sababu kupewa jina la Mtende na Makunduchi. Kazi zote hizi ni muhimu kwa utafiti huu.

Mlacha na Hurkeinein (1995), wameeleza asili ya mitaa inayopatikana kisiwani Pemba. Uvuani, asili yake walihamia wageni wakawa wanafanya shughuli za uvuvi, wakaja watu wakawauliza ‘Uvuani’ maana unavua nini? Hapo ndipo kijiji hicho kikaitwa Uvuani. Micheweni, walikuwapo watu makatili, wenye tabia ya kuwaua watu. Hivyo, watu walioishi mbali na eneo hilo walipaita Michawini linatokana na Uchawini lenye maana ya kuuwa, baadaye, pakaitwa Micheweni. Hii ni kazi ambayo imesaidia kuchambua kipengele cha ujumbe.

Seif (2011), ameeleza asili ya mitaa iliyopo Morogoro, Gairo asili yake ni Kigairo (yaani sehemu ya kugawiana vitu) sehemu hiyo hapo zamani, Watemi walitumia kugawiana meno ya ndovu, Wakaguru walikuwa wanasema ‘chikututa chigairo’. Maana tunakwenda sehemu ya kugawiana. Baadaye likawa Gulio, soko la jumla na rejareja. Misingisi ni jina lililotokana na mti wa asili wa Kikaguru unaoitwa Msingisi. Mkalama, linatokana na Rambo la kunywesha maji mifugo. Kikaguru huitwa ‘Ikalama’ Wakaguru walikuwa wanapokwenda kunywesha mifugo yao wanasema, ‘Chikuruta Mkalama’ yaani tunakwenda Mkalama. Uasili wa majina ya mitaa ni muhimu katika uchambuzi wa kazi hii.

Ndamba (2013), ameelezea asili ya Wabungu, chimbuko lao kutoka Kusini ya Afrika, waliingia Tanzania upande wa Mashariki mpaka sehemu ya Tukuyu, Songea hadi Morogoro. Walikaa kwa muda mrefu na kuacha alama za majina Ilonga, lenye maana, Mwenye (kiongozi wa Wabungu). Waliendelea na safari hadi Bonde la ufa la Mashariki na kuingia Ukimbu na Kwimba, hapo waliwakuta wenyeji wao Wanyamwanga ambao walikuwa hawana uongozi thabiti waliwafukuza kwa urahisi. Walikwenda Kapalala linalotokana na neno Koupala lenye maana, kunoa ni sehemu ya kunolea mikuki na silaha za kivita za asili. Baadaye walishuka ndani ya bonde la ufa katika kijiji cha Uinde. Linalotokana na neno Toundinde kwa Kibungu maana yake tuzuwie kijiji hiki. Majina yote haya yanatoa maana inayofahamika na wanajamii.

Mbijima (2011), alitafiti dhima ya visasili katika jamii ya Wagogo. Alieleza asili ya Dodoma, kulikuwa na Mzungu aliyeitwa Spreling, alikuwa na bustani kubwa yenye maji mengi. Siku moja, alikuja ndovu kunywa maji lakini alididimia katika ardhi. Hivyo mtumishi wake alisema, nhembo idodoma, mzungu akasema, Dodoma. Pia ameeleza, mtaa wa Mahoma maana yake ni kuchoma mkuki, linatokana na wakaazi wake kuwa wapiganaji. Asili ya Msalato, linatokana na mti unaoitwa msalato. Mkonze, linatokana na mti wa mkonze na Kikuyu linatokana na jina la mti wa mkuyu. Maelezo hayo yanaonesha, majina hutolewa kutokana na sababu za kimazingira na matukio yanayotokea katika jamii.

Bakiza (2011), wametaja majina ya mitaa inayopatikana mjini Unguja, Sehemu alizokuwa akiishi mwandishi mashuhuri, Mohammed Said Abdalla (Bwana MSA). Wametaja shughuli zilizokuwa zikifanya katika mitaa hiyo. Kundemba, palikuwa

maarufu kwa pombe za kienyeji na ngoma ya mbwa kachoka (beni) pamoja na sherehe na tafrija. Baraste kipande, ulikuwa mtaa wa kukutanisha tamaduni za majumba ya mawe na Ngambu. Kachorora, kulikuwa na mashindano ya ngoma za kienyeji, benibati, kilua na kibisa. Mwembetanga, mtaa wa mapembea watoto walikwenda kwa ajili ya burudani wakati wa jioni. Maelezo haya yatamsaidia mtafiti kuwaelewa kwa undani watu wa Unguja, kwani ili mtafiti aweze kuitafiti jamii lazima ajue ndani nje, silka, utamaduni, mila na dasturi zao.

Kipindi cha Redio Nour (2013), kimesimulia asili ya mitaa inayopatikana kisiwani Pemba. Kijiji cha Tasani, kilipawa jina hilo, kwa sababu lilikuwa eneo dogo lenye kukaa maji. Wema na waje, ni mtaa uliokuwa ukikaliwa na Waarabu weusi, waliojitenga na watu. Wakiishi peke yao, wakawa wanasema. Sisi tuko huko wema na waje. Asili ya Kiuyu, alikuwapo bibi aliyeitwa Bi Kirembwe. Alikuwa haelewani na watu kwa sababu ya tabia yake mbaya ya ushirikina. Hivyo, alitengwa na watu. Baadae, aliamua kuhama, lakini kutokana na tabu alizopata huko, alirejea tena kijijini. Watu walipomuona walisema jamani kile kibibi, Kiuyu maana karejea. Kazi hii imesaidia kujua kuwa majina ya mitaa yanaendana na matukio ya kila siku katika jamii.

Zanzibar Broadcasting Cooperation (2014), imeeleza asili ya majina ya mitaa ya Unguja, inayotokana na majina ya mifereji. Mfereji wa wima ni mfereji mrefu uliyowekwa miaka ya sitini, mara tu baada ya Uhuru. Mfereji wa Kiambazani, upo katika kiambaza cha nyumba ya mtu aliyejitolea nyumba yake kuwekwa mfereji. Mfereji Maringo ni mfereji uliopo juu ya kilima unaotoa maji kidogo kidogo ndio sababu ya eneo hilo kupewa jina hilo. Rahaleo, zamani pakiitwa Miafuni, baadaye

paliengwa jengo la Kariakoo likatiwa mapembea na vikajengwa vyoo vya wanawake na wanaume watu wengi wakawa wanapokwenda kutembea, wakisema tunakwenda Rahaleo, lenye maana ya raha za kileo. Kutokana na maelezo yote hayo, ni dhahiri kuwa, majina mengi yana maana, chanzo na sababu.

2.1.2 Asili ya Koo

Mwaruka (1965), alieleza juu ya ukoo wa Pazi. Wajukuu zake waliitwa kina Pazi. Alieleza mgawanyiko wa koo katika Uzaramu. Koo ziligawika kutokana na makabila na masimulizi maalumu yanayojulisha asili ya koo hizo. Ziko koo zilizotokana na makabila mengine. Koo zilizotokana na majina ya watu kwa sababu ya matendo yao na koo zilizotokana na majina waliyopewa na majirani zao. Mfano ukoo wa Wamindu, walihama kutoka nchi ya Zigua, kwa sababu ya kukimbia vita vya kikabila. Walisema wao, wemetokana na mlima wa Mindu uliyopo Morogoro kuelekia Kilosa. Kwa ajili hiyo, wakaazi wa eneo hilo wakaaitwa Wamindu. Kwa maelezo hayo, mtafiti amepata kujua miongoni mwa njia zinazotumika katika kutoa majina ya koo.

Rashid (2013), ameeleza asili ya Wahiyao. Jina hili linatokana na mlima, Yao uliyopo kati ya Muembe na Mto kuchilingo, nchini Msumbiji. Ni mlima wenye mbuga. Wahiyao walikuja Tanzania katika makundi mawili, kundi la kwanza, lilipita mto Ruvuma kushuka Newala na Masasi. Kundi la pili, lilipita Malawi hadi Mkoa wa Ruvuma kuingia Tunduru. Huko kwao walikimbia vita vya makabila kati yao na Wangoni ambao waliwafukuza Wahiyao katika vita vinavyoitwa “Ngondoja Makwangala” yaani vita vya uasi. Dosha (2010), ameeleza asili ya Waha ni nchi

jirani za Burundi, Ruwanda na Kongo. Jamii ya Waha, iliingia Tanganyika katika vikundi vidogo vidogo miaka mingi iliyopita na lugha waliyokuwa wakitumia ni Kiha ambayo asili yake ni Kinyaruanda, ikiwa na maana ya watu wanaotumia lugha moja. Hivyo kabila la Waha linatoa picha ya umoja na mshikamano. Mdee M. Masabo (2002), wameelezea historia ya Wazigua Somalia. Asili yao ni Handeni. Walihamia Somalia kwa kukimbia njaa kubwa iliyojulikana kama Gumbodya. Kidyanchinga, yaani njaa ya kula ngozi. Wameeleza maana ya majina ya miji ya Uzigua, ya Somalia. Kama vile, Kismayuu, lenye maana ya kisima cha juu. Mbulyaga na Mbulizaga, maana yake, mambo juhudi au habari zote zimepotea. Wazigua waliposhindwa kurudi Handeni, walikata tamaa.

Hivyo, walianzisha miji na kuipa majina hayo kuonesha, kuwa juhudi za kurudi nyumbani zilishindikana. Mkalangoni, mji wa Wazingua wenye maana, mahali ambapo wasomali walipigwa. Wasomali walipaita hivyo, ikimaanisha ukoo uko wapi? Au Tumekosa ukoo yaani wamemalizwa kwa kupigwa vita na Wazigua. Gombweni, jina la mji wa Wazigua unaohusishwa na Bweni, ambalo ni jina la eneo huko Pangani Tanga. Zunguni, mahala ambapo akiishi Mzungu Toley ambaye ni miongoni mwa watawala wakati huo. Tunaona kuwa, majina ya miji na vijiji vya Somalia yanaakisi yale ya Uzigua na vijiji vya Waswahili kutoka pwani ya Tanga na Bagamoyo ambayo yanatoa maana.

Mussa (1980), Kivenule (2013) wamesimulia asili ya Wahehe. Koo nyingi za Kihehe, zipo kutokana na tabia tafauti za kimaisha. Majina ya koo, yalibeba maana nzima ya kihistora na shughuli zinazofanywa na jamii. Mfano, koo za Wahehe za awali ni Wigawilo, Wahafiwa, Wanyandevulwa na Wategela waliokuwa mafundi wa

kupata na kufua chuma. Jina la ukoo wao, lina maana ya wafukutaji, kwani wakitumia mifukuto kupulizia moto kwenye tanu za kuchomea mchanga ili kupata chuma. Koo zilizokuwa maarufu katika upiganaji wa vita, ndani ya himaya ya Wahehe ambazo majina yake yalitoa maana ya ushujaa na ujasiri. Mfano, Kivenule, lina maana ya sifa ya ujasiri vitani, hasa katika kutumia silaha za asili. Kuhoma, maana yake, kuuu au kufyeka maadui. Kuna majina yaliyotokana na mfululizo wa majanga ya asili. Mfano, Mponela, maana yake kupona. Mwanitu, alizawa kweusi kwa kutumia lungali ili kuwasha moto wa kumulikia, Luhanage, maana yake ni kuugua sana. Mgendwa, aliyezaliwa kwa taabu. Mbinu zilizotumika katika kutoa majina ya koo yamesaidia kugundua asili ya majina ya mitaa.

Chomboz (2014), wamemnukuu Ndumbaro akielezea asili ya Wamatumbi wanaoishi Wilaya ya Kilwa, Mkoa wa Lindi, eneo wanaloishi ni Milimani. Kwa kilugha neno Itumbi, maana yake, watu wanaoishi milimani. Wengi wao wakitokea Ungonini, baada ya kukimbia vita vya uasi, waliitwa nzalendo yaani wenyeji. Majina yao ya ukoo hurithishana kizazi hadi kizazi, ambayo huwa yana maana katika jamii. Kibaga, mtu asiyepigika yaani mwenye nguvu, Ngemba asiye na chakula, Liboi, mtu muoga, anayetoweka kwa urahisi panapotokea vita, Likaino maana yake mnajisumbua bure. Kazi hii inadhihirisha kuwa majina yana maana inayofahamika na wanajamii wenyewe.

Mwalugaja (2013), ameelezea asili ya Mbeya ni neno la Kisafwa lenye maana ya Ibheya likiwa na maana ya chumvi. Wafanyabiashara walifika eneo hilo na kubadilishana chumvi kwa mazao mengine na wenyeji wa eneo hilo. Mji wa Mbeya, ulianzishwa wakati wa Wakoloni (1927). Tukuyu, eneo lililokuwa na miti mingi ya

Mikuyu. Wanyakyusa walikuwa wanapita katika sehemu hiyo na kusema, “Patukuju” yaani pahala penye miti ya Mikuyu. Kutokana na lafudhi ya Wanyakyusa kwao, ilikuwa rahisi kutamka Tukuju. Baadaye, ilibadilika na kuwa Tukuyu. Mji ulio Kusini mwa jiji la Mbeya, katika barabara, iendayo Mji wa Mbamba Bay na nyengine kuelekea Malawi. Kutokana na maelezo hayo, majina katika jamii nyingi za Afrika, hutolewa kwa kufuata kaida za kijamii ambazo huonesha mawazo na tajiriba za kijamii, hubeba maana na hutoa ujumbe.

2.1.3 Majina ya Semi

Hizi ni kazi ambazo zinahusu majina ya vitu mbalimbali kama vile majina ya kanga, majina ya gari, mikoba, tiketi za daladala na bajaji ambazo zimechambuliwa kifasihi kwa kuangaliwa vipengele vya fani na maudhui.

Mtoro (2011), alichunguza majina yaliyoandikwa katika daladala, alichambua vipengele vya lugha na ujumbe. Alieleza kuwa, majina hayo huwa yanatoa ujumbe maalumu kwa jamii. Mfano, “maisha ni safari ndefu,” maisha ni muda wa uhai kwa kiumbe na safari ni tendo la kwenda mbali. Hivyo, majina hayo yanafunza kuwa, binaadamu anatoka hatua moja kwenda nyengine kiakili na kimwili, binadamu hupambana na vikwazo vingi katika maisha yake. Hassan (2010), alieleza asili ya neno daladala linatokana na nauli ya awali ya mabasi ambayo hapo mwanzo ilikuwa ni shilingi tano, ikijulikana ‘dala’ kwa kuwa na thamani sawa na dolla moja ya Kimarekani. Kutokana na kurudiarudia kwa makonda neno dala, ndipo lilipopatikana neno daladala. Pia, alichunguza mitindo ya matumizi ya lugha kwa majina yaliyoandikwa katika bajaji. Aliangalia lugha ya sitiari. Mfano ‘Subira ni ufunguo wa riziki’, Mtu kwao, Mtu kazi. Tash biha, ‘hata mbuyu ulikuwa kama mchicha’

Tashhisi, Ukimwi mwenda kasi unaua. Kazi hizo zimetoa mchango mkubwa katika utafiti huu kwa kuonesha matumizi ya lugha na ujumbe.

Moh'd (2009), amechambua majina katika gari za abiria kwa kuangalia ujumbe uliopatikana katika maandishi hayo. Ameyagawa majina hayo katika makundi matatu. Kwanza majina ya kisiasa. Mfano, Ari mpya, umoja na mshikamano, sote ni wamoja. yanahimiza jamii kuwa pamoja na kuepuka ubaguzi na utengano. Pili, majina ya kiuchumi. Mfano, hatulali njiani, Mwisho wa jitihada ni mafanikio, Usife moyo, maskini hachoki. yanahimiza juhudi na bidii katika kufanya kazi. Tatu, majina ya kijamii. Mfano, 'Nani kama mama?' Ulezi kazi, Mkanye mwanao, Wema hauozi. yanahimiza umuhimu wa malezi mema kwa watoto ili wawe vijana wema watakaokuja jenga Taifa lao. Chande (2014), amechunguza majina ya kanga na ameeleza kuwa majina ya kanga yanapatikana kutokana na picha au mafumbo yanayotoa ujumbe maalumu. Mfano, kanga yenye picha ya kasuku huitwa *kasuku*, kanga yenye fumbo la, kikulacho ki nguoni mwako, huitwa *kikulacho* ikimaanisha kuwa adui yako yuko karibu nawe. Kazi hii imesaidia katika kuchambua ujumbe wa majina.

Pengo la Utafiti

Baada ya kutalii kazi za wataalamu mbalimbali. Mtafiti amegundua kuwa, watafiti wengi waliochunguza majina wamejikita zaidi katika upande wa lughawiya kwa kuchunguza mifumo inayotumika kuunda majina bila ya kuhusisha majina hayo katika kipengele cha fasihi. Hivyo, utafiti huu umekusudia kutafiti fasihi ya majina ya mitaa ya Mjini Unguja kwa kuchunguza asili ya majina ya mitaa, mitindo, lugha

iliyotumika kuunda majina ya mitaa, na mwisho kubainisha ujumbe wa majina ya mitaa ya Mjini Unguja.

2.1.4 Hitimishi

Katika utafiti huu mtafiti alitalii maandishi kutoka maktaba, tasnifu na wavupepe. Kazi ambazo ziliandikwa asili na uchambuzi wa majina na mtindo katika kipengele cha lugha. Taarifa zilizopatikana zimesaidia kubainisha jinsi majina yalivyochambuliwa pia zimetumika katika kujenga mwega wa kazi hii.

2.2 Uhakiki wa Nadharia

Nadharia ni kauli za kitaalimu, zinazotolewa na wasomi na wataalamu baada ya kufanya utafiti wa kina. Nadharia inaweza kuundwa kutokana na tajriba ya mtu binafsi au juhudi za kikundi cha watu. Sengo (2009), amesema nadharia ni wazo kuu, fikra kuu, mwongozo wa mtu au watu, wa pahala fulani, wakati fulani, kwa sababu fulani. Simiyu (2011), nadharia ni mwongozo unaomuelekeza mpokezi wa kazi ya fasihi kuifahamu kwa undani zaidi. Ni kama dira ambayo inawapa wapokezi vigezo sawa vya kuzitathmini kazi za fasihi. Doorewoard (2005) amesema nadharia ni njia inayotumika kumuongezea mtafiti uoni zaidi kwa kupata elimu ya msingi au ya awali ambayo humuongoza mtafiti katika kazi yake. Hivyo, utafiti huu utaongozwa na nadharia ya uhalisia na nadharia ya ndani mnje.

2.2.1 Nadharia ya Uhalisia

Chimbuko la nadharia hii linahusishwa na kipindi maalumu cha kihistoria katika jamii za Ulaya. Kipindi hiki kilianza mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa nchini Ufaransa na kuhusishwa na waandishi kama Balzae, Stendhal na blaubart. Waandishi

hawa walisisitiza maandishi ya kikweli kwenye kazi zao. Msingi mkuu wa nadharia hii ni usimulizi wa matukio kama yanavyotokea katika ulimwengu halishi au kwa namna inayokaribiana. Kwa hivyo, mwanafasihi anapaswa kuyaakisi maisha ya kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa kwa kutoa picha za wahusika, matukio na mandhari ambayo yanaoana na uhalisia wa jamii. Mwandishi atilie mkazo wahusika katika hali za kawaida za maisha, matukio na mandhari ya kawaida au yanayoweza kuonekana katika jamii. Huu ndio msingi hasa wa kauli ya Lenin kuwa "Fasihi ni kioo cha lugha" Kwa kiasi kikubwa tunaweza kusema kuwa jinsi ya kusawiri na kuelezea uhalisia hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyengine, kila kizazi huwa na uhalisia wake.

Fasihi ina kazi ya kuyaweka matukio ya kijamii katika ulimwengu wa kawaida na wa kweli ambao unaeleza uhalisia wa yale yanayotendwa (Senkore na Kahigi, 2007). Fasihi ni taasisi ya jamii na uhusiano wake na jamii hauwezi kutenganishwa. Escarpit (1974) amesisitiza fasihi ichukuliwe kama ilivyo na uhusiano wake na maisha ya jamii, moja ya kazi ya fasihi ni kuhifadhi historia ya jamii. Kwa kuchunguza kazi za fasihi, tunaweza kupata historia ya jamii katika vipindi tafauti. Mfano, tukiangalia mtaa wa Kisiwandui na Darajani tunaweza kuona hali ya mazingira ya bahari iliyokuwa imezunguka eneo hilo kabla ya kufukiwa na kuwa makaazi ya watu sasa. Majina ya Muungano, Mzalendo na Nyerere yanahifadhi historia ya wakati wa Uhuru na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar

Hivyo, mtafiti anaona kauli ya kuwa fasihi ina mahusiano na maisha ya jamii, ni hoja yenye mashiko. Nadharia hii imesaidia utafiti kuchunguza asili ya majina ya mitaa ambayo yanatupa hali halisi ya maisha yetu hapo kale kisiasa, kiuchumi, kijamii na

kimazingira. Tatizo la nadharia ya uhalisia ni kuwa msingi wake mkubwa ni kuzungumzia mambo kihalisia, jambo ambalo limezua mjadala mkubwa kwa wananadharia wa kisasa kwani wao wanaamini kuwa mwanafasihi anao upeo mkubwa wa kutumia mbinu tofauti katika kuyasawiri mazingira, wahusika na hata lugha. Hivyo mtafiti ametumia nadharia ya ndani nje ili iongoze utafiti katika kuchambua mtindo, lugha na ujumbe wa majina ya mitaa ya Mjini Unguja.

2.2.2 Nadharia ya Ndani –Nnje

Nadharia ya ndani nje ni moja ya nadharia kongwe za sanaajadiiya. Licha ya kuwa ina historia ya muda mrefu, kumekuwa na mfululizo wa mabadiliko ya matumizi ya nadharia hii. Yurilong katika makumbusho ya Taifa ya Marekani anabainisha chimbuko la nadharia hii kuwa, katika karne ya kumi na tatu wataalamu wa sayansi inayohusu mwili wa binadamu wakishirikiana na wanataalimu wa sanaa za maonesho, walitengeneza jukwaa linaloonesha ushirikiano wa kimasomo kati ya wanafunzi wa sayansi na wale wa sanaa. Mchakato huu unatufikisha katika karne ya kumi na nane ambapo mwanataalimu Bell (1806) alielezea umuhimu wa sayansi inayohusu mwili na viungo vyake jinsi vinavyohusiana na namna mwanadamu anavyoelezea hisia zake. Miaka mingi imepita na wanataalimu wengi wameitumia nadharia hii katika mambo mengi kama vile sheria, biashara, uchumi na hata fasihi.

Sengo (2009) amesisitiza, mtafiti, mwalimu au mhakiki wa fasihi ya jamii fulani, ili aweze kuitafiti, kuifundisha na kuihakiki ni shuruti aitambue vizuri. fasihi ya jamii husika ndani nje. Sengo (ameshatajwa) ameigawa nadharia hii katika hali kuu mbili. Nadharia ya fani ambayo katika kazi ya fasihi kuna lisemwalo na namna ya kulisema, mbinu, mtindo na uzungumzaji wake. Pili, nadharia ya dhima na kazi.

Kazi ya fasihi katika jamii ni kumshawishi mwanadamu kutumia lugha yake kwa umahiri. Nadharia hii inabainisha jinsi fani na maudhui zinavyotegemeana kila kimoja ni muhimu kwa chenzake. Majina ya mitaa ya Mjini Unguja yanahitaji darubini ya kuyamurika ndani nje ili uweze kugundua fasihi iliyomo ndani ya majina hayo. Hivyo, nadharia hii imeongoza utafiti katika kuyachunguza majina ya mitaa ya Mjini Unguja ili kubainisha mtindo, lugha na ujumbe unaopatikana katika majina ya mitaa ya Mjini Unguja.

2.2.3 Hitimishi

Katika sehemu hii mtafiti ameeleza kwa uwazi nadharia za sanaajadii ambazo ni muhimu katika utafiti huu. Kuna nadharia nyingi katika sanaajadii lakini mtafiti amechagua nadharia mbili na kufafanua. Nadharia zilizotumika ni nadharia ya uhalisia ambayo imesaidia katika uchambuzi wa asili ya majinaya mitaa ya Mjini Unguja na nadharia ya ndani nje imetumika katika kuchambua mtindo, lugha na ujumbe wa majina ya mitaa ya Mjini Unguja.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Kabla ya kuanza kazi ya utafiti kwanza kabisa, kazi kubwa ni kupangilia kuhusu namna utafiti utakavyofanywa. Mpangilio huo ndiyo unaoitwa usanifu wa utafiti. Hapa mtafiti anapaswa kupanga nini, wapi, lini na kwa namna gani utafiti utafanyika. Kwa maneno mengine usanifu wa utafiti ni mpangilio na utaratibu wa kukusanya na kuchambua data katika mpangilio maalumu bila kupoteza lengo kuu na madhumuni ya utafiti (Dekeba, 2012). Hivyo, ndivyo ilivyo katika utafiti, mtafiti anahitaji kuwa na mpango kabla ya kwenda kukusanya data unaobainisha mtiririko wote wa utafiti uliokusanya mbinu za utafiti, eneo la utafiti, vifaa vya utafiti na uteuzi wa watafitiwa.

3.2 Mbinu za Kukusanyia Data

Opie (2010), mbinu za utafiti ni dhanna au hatua za kitaalimu za kupatia taarifa kwa kuzingatia njia ambazo zitasahilisha kupata data za uhakika kuhusiana na utafiti unaofanyika. Kwa hiyo, mbinu za utafiti, ni ujuzi na ufundi anaotumia mtafiti, ili kupata wepesi wakukusanya data. Utafiti huu umehusisha mbinu ya usaili na hojaji, ambazo kwa pamoja, zimerahisisha ukusanyaji wa data.

3.2.1 Mbinu ya Usaili

Usaili ni mbinu inayohusisha kujieleza kwa mdomo katika kuuliza na kujibu maswali. Mbinu hii, humuezesha mtafiti kusaili watu binafsi au kikundi maalumu, maswali madogo madogo yanayohusu suala lake la utafiti (Simiyu, 2011). Usaili

huu, umeendeshwa katika hali ya nusu fungu, kwa baadhi ya maswali kutayarishwa kabla ya usaili na mengine, kutolewa na mtafiti papo kwa papo, maswali ya ziada, ambayo hayakuorodheshwa katika orodha ya maswali ya usaili. Hivyo, maswali yalitayarishwa na kuulizwa ili kupata ufafanuzi. Njia hii iliwahusisha wazee wasiojua kusoma na kuandika kwa kujibu maswali tu waliyolizwa Njia hii ni nzuri kwani imemsaidia mtafiti kupata taarifa za ziada zilizotolewa na watafitiwa baada ya mtafiti kuwauliza maswali ya ziada uso kwa macho.

Denscombe (1998), ametahadharisha kuwa msailiwa anaweza kujiona amekerwa au kujisikia vibaya kujibu maswali, mtafiti anatakiwa kujiamini na kuwa makini. Baadhi ya watafitiwa walikuwa wanahisi kupotezewa muda wao kwa kufanyiwa usaili lakini mtafiti alilainisha tatizo hili kwa kutumia maneno laini yaliyomtoa nyoka pangoni kwani kuagiza kufyekeza na kuonana ni kuelewa.

3.2.2 Mbinu ya Hojaji

Hojaji ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambayo mtafiti huandaa orodha ya maswali yanayoelekeza namna ya kujibu na hutolewa kwa watafitiwa ili wayajibu (Enon, 1998) Mtafiti ametumia hojaji kama njia ya ukusanyaji wa data kwa kuandaa maswali yanayotarajiwa kujibiwa na watafitiwa ili kupata habari inayohitajika katika utafiti huu, mtafiti aliandaa hojaji ambazo zina maswali mchanganyiko yaliyolenga malengo ya utafiti. Hojaji hizi walipewa viongozi ambao wanajua kusoma na kuandika Mbinu hii inafaa kwa sababu inasaidia katika ulinganishaji wa taarifa zilizopatikana kwa watafitiwa ili zifanyiwe tathmini na kukamilisha ithibati za utafiti.

Mbinu hii inatumia muda, pesa, ucheleweshaji wa kurudishwa kwa mahojaji au kurudishwa bila kujibiwa, hali hiyo inaweza kumfanya mtafiti kushindwa kupata taarifa za kutosha. Hivyo mtafiti alichapisha mahojaji mengi zaidi ili kutatua matatizo hayo, na wasaidizi wa mtafiti walitumika kubeba mahojaji, kuwahoji watafitiwa, ama wao kusimamia ujazaji au wao wenyewe kujaza majibu, kisha kukusanya mahojaji hayo yote, na kumrudishia mtafiti.

3.3.3 Mbinu ya Mtafiti Msaidizi

Sevenye (2001) amesema mtafiti msaidizi ni njia ambayo mtafiti anatumia ili aweze kusaidiwa kila asichokifahamu au vigumu utekelezaji wake. Kwavile, mtafiti ni mgeni katika baadhi ya mitaa, alitafuta wasaidizi ambao ni wenyeji wa maeneo hayo wanaotambulika na jamii. Kazi ya wasaidizi ilikuwa ni kumtambulisha mtafiti kwa watafitiwa na wengine walitumika katika kujaza hojaji pale ambapo palikuwa na ugumu wa kuwapata watafitiwa uso na macho. Watafiti wasaidizi waliotumika ni masheha ambao walimtambulisha mtafiti kwa watafitiwa na makatibu wawili ambao walimsaidia mtafiti kujaza hojaji baada ya kupata mafunzo kutoka kwa mtafiti. Njia hii ilisaidia sana kufanikisha kazi ya kukusanya data kwa wepesi licha ya kuwa na urasimu wa kuwapata watafiti wasaidizi lakini mtafiti alijitahidi kuwa mpole na mwenye uvumilivu.

3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyika Wilaya ya Mjini Unguja, ambako ndiko kitovu cha Makao Makuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mji wa Manispaa ya Zanzibar. Wilaya ya Mjini ni miongoni mwa wilaya zinazounda Mkoa wa Mjini\Magharibi. 27Wilaya hii, kwa Magharibi na Kusini, imepakana na Wilaya ya Magharibi na

upande wa Mashariki imepakana na bahari ya Hindi, takwimu za Sensa za vipindi tafauti zinaonesha kuwa idadi ya watu, ndani ya wilaya hii, inaongezeka siku hadi siku kutoka watu 68,380 mwaka 1967 hadi watu 223,033 mwaka 2012. Mgawanyo wa idadi ya watu unaonekana katika jedwali.

Jedwali Na 3.1: Idadi ya Watu wa Mkoa wa Mjini

Wilaya	Idadi ya Watu				
	1967	1978	1988	2002	2012
Mjini	68,380	110,506	157,634	206,292	223,033

Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu wa Serikali (2013)

Wilaya hii ina ukubwa wa kilomita za mraba 16 zilizogawika katika majimbo kumi ya uchaguzi ambayo ni Mjimkongwe, Kikwajuni, Rahaleo, Jang'ombe, Kwahani, Magomeni, Mpendae, Amani, Chumbuni na Kwamtipura. Kuna Wadi 20 na shehia 45 zenye idadi ya watu 223,033 wakiwamo wanaume 106,11 na wanawake 116,422 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012.

Wilaya hii, kiuchumi inategemea shughuli za biashara, utalii, uvuvi na ajira za serikali na binafsi kwa lengo la kujipatia kipato kwa wakaazi wake ili kukidhi mahitaji ya kila siku. Mkoa huu ni kitovu cha shughuli za kiuchumi kwa Mikoa yote ya Zanzibar, kwa vile una miundombinu ya bandari na barabara zilizotoka sehemu za mashamba kuja katika masoko makuu ya kuuzia na kununulia bidhaa. Lugha ya Kiswahili ni kieleza cha utamaduni wa watu wa Unguja, lugha hii imesheheni misemo, mafumbo, nyimbo, vitendawili, majina ya watu na majina ya mitaa yanayo gusa kila uwanja wa maisha ya Waswahili.

Mtafiti ameteua maeneo hayo kwa sababu ni maeneo ambayo majina ya mitaa ya asili bado hayajaathirika na makuzi ya miji, yaliyopelekea kutolewa kwa majina

mapya yasiyorandana na utamaduni wa kizanzibari, vile vile, kuna mitaa mingi na watu wengi ambao ni wenyeji wanaofahamu historia ya maeneo hayo.

3.4 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umechunguza fasihi ya majina ya mitaa ya Mjini Unguja. Katika majina hayo kumechunguzwa kipengele cha asili ya majina hayo, mtindo na lugha iliyotumika kuunda majina ya mitaa na ujumbe unaopatikana katika majina ya mitaa ya Mjini Unguja.

3.5 Uteuzi wa Watafitiwa

Prewitt (1980) amesema watafitiwa ni idadi au sehemu ndogo inayotokana na kundi kubwa la watoa taarifa wanaochaguliwa kuwakilisha kundi kubwa. Watafitiwa walioteuliwa katika utafiti huu, kwa niaba ya jamii nzima, walioshiriki kutoa taarifa, ni viongozi wa kiserikali wakiwamo wakurugenzi, Mkuu wa Mkoa na masheha pamoja na wazee mashuhuri wanaotambua historia. Mtafiti ameteua idadi ya watafitiwa hamsini (50) kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Enon (1998), amesema kuwa, uwakilishi wa kundi dogo la watu ambao anawatumia mtafiti ni ile hali ya kuchagua wawakilishi kwa kuzingatia malengo maalumu. Utafiti huu ulijumuisha kundi dogo ambalo lilizingatia utambuzi wao wa mambo katika jamii. Cohen na wenzake (2000), wamesema katika kuwakilisha kundi dogo la watafitiwa, kila mmoja atakuwa na nafasi sawa na mwenzake. Mtafiti ameteua makundi mawili ya watafitiwa ili kupunguza muda, Waliohojiwa ni:

Wazee: Mtafiti amechagua wazee wa umri wa miaka (40-80) amewachagua hawo kwa sababu wameshakuwa na uzowefu mkubwa wa maisha na wanaofahamu mambo

mengi ya kihistoria. Mtafiti alitumia uteuzi lengwa (purposive sampling), baada ya kupata taarifa zao kupitia kwa masheha ili kupata data maalumu ambazo watafitiwa aliowachagua wanazo. Kothari (2009), amefafanua, uzuri wa utafiti ni kwa mtafiti kuchagua watafitiwa kulingana na madhumuni maaalumu.

Viongozi: Hawa ni watu wenye mamlaka ya kiserikali katika Mji. Mtafiti amewachagua wao kwa sababu baadhi yao wanafahamu historia za Miji. Vile vile, mtafiti amewatumia Masheha ili kumsaidia katika kuwapata wazee wanaofahamu mambo ya kihistoria. Uteuzi wa masheha umetumia njia ya uteuzi wa sampuli wa kimfumo (systematic sampling). Katika njia hii mtafiti anatumia mfumo maalumu katika kuwapata watafitiwa. Kwa mfano, baada ya kwenda nyanjani anaweza kumhoji kila mtu wa nane katika idadi ya kundi la watu. Mtafiti aliorodhesha majina ya shehia 45 zinazopatikana Mjini Unguja. Kisha alihesabu moja mpaka tatu, shehia zilizopata namba tatu ndizo alizozitumia kwa ajili ya utafiti. Hivyo, aliwahoji masheha 18 na Mkurugenzi wa Shirika la Utalii pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Unguja kwa kutumia uteuzi lengwa baada ya kupata taarifa zao kupitia kwa masheha.

Jedwali Na 3.2: Uteuzi wa Watafitiwa

JIMBO	VIONGOZI		WAZEE		
	MK	MM	MK	MM	JUMLA
Jang'ombe	03	03	05	05	16
Rahaleo	03	03	05	05	16
Mji Mkongwe	04	04	05	05	18
Jumla	10	10	15	15	50

Chanzo: Mtafiti (2014)

3.6 Njia ya Uchambuzi wa Data

Mtafiti alitumia mkabala stahilifu katika uchambuzi wa data, ambao ni ule, unaotumia maelezo katika kuchambua data, mkabala huu umechaguliwa kwa sababu data zilizokusanywa ziko katika hali ya maelezo. Kwa vile, lengo la utafiti ni kuchunguza fasihi ya majina ya mitaa, hivyo, data zote zilizochambuliwa zimechambuliwa kwa njia ya maelezo ili kufikia lengo.

3.7 Hitimishi

Kwa ujumla sura hii imeelezea mbinu za utafiti zilizotumika, ambazo ni mbinu ya usaili na hojaji kwa kugusia faida na changamoto alizokabiliana nazo. Pia, alielezea eneo lililofanyika utafiti, katika mitaa inayopatikana Mjini Unguja na mwisho mtafiti alielezea uteuzi wa watafitiwa kwa kutumia njia ya kimfumo na njia ya uteuzi lengwa.

SURA YA NNE

UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti amewasilisha na kufanya uchambuzi wa majina ya mitaa inayopatikana Mjini Unguja, jumla ya mitaa 75 imechambuliwa. Uchambuzi huu umezingatia kufafanua fasihi ya majina ya mitaa kifani na kimaudhui. Mtafiti ameyagawa majina hayo katika makundi manne nayo ni: Majina yanayotokana na miti (34), majina yanayotokana na watu (10), majina yanayotokana na mazingira (10), majina ya matukio (19). Majina hayo yamekusanywa na kuainishwa kama ifuatavyo:

4.2 Asili ya Majina ya Mitaa

Madhumuni maalumu ya kwanza ni kuchambua asili ya majina ya mitaa inayopatikana Mjini Unguja. Neno asili lina maana ya chanzo, au jinsi jambo lilivyoanzia au lilivyotokea.(SAMIKISA 2012) kwa hivyo tunapoangalia asili ya majina tunaangalia jinsi majina hayo yalivyopatikana au yalivyoanza. Mtafiti ameelezea asili ya majina ya mitaa kwa kuyagawa majina yanayotokana na miti, majina yanayotokana na watu, majina ya mazingira na majina ya matukio.

4.2.1 Majina Yenye Asili ya Miti

Mtafiti ameyagawa majina yenye asili ya miti katika mikabala mitatu: Majina yanayotokana na muembe, majina yanayotokana na mbuyu na majina mengineyo kama yanavyoonekana katika majadweli.

Jedwali Na 4.1: Majina ya Miti

Muembe	Mtaa
Muembe	Mwembeladu, Mwembenjugu, Mwembebeni, Mwembekisonge, Mwemberikunda, Mwembetanga, Mwembeshauri, Miembeni, Mwembemadema, Mwembemakumbi, Mwembemimba, Mwembedezo, Mwembemchomeke, Kiembe samaki na Muembematarumbeta
Mbuyu	Mbuyupacha, Mbuyu taifa, Mbuyukidambwita, Mbuyumnene, Mbuyuni
Mengineyo	Migombani, Mkunazini, Mikunguni, Mshelishelini, Misufini, Michenzani, Mtendeni, Mkamasini, Kinazini, Mfenesi mazizi, Tomondo, Mlandege, Mkungumalofa, na Kikwajuni

Chanzo: Mtafiti (2014)

4.2.1.1 Majina Yanayotokana na Miti

Mitaa inayopatikana Mjini Unguja, mingi yao imetokana na majina ya miti kama vile miembe, mibuyu na miti mingineyo. Mtafiti ametumia nadharia ya uhalisia katika kuchambua data kwani majina hayo yamepatikana kutokana na hali halisi ya wakati.

4.2.1.2 Mwembe

Mwembe ni mti mkubwa wenye matawi mengi yaliyojitawanya na majani marefumarefu unaozaa matunda ya embe (TUKI, 2010). Majina yenye asili ya mwembe ni Miembeni, Mwembeshauri, Mwembemadema, Mwemberikunda, Mwembeladu, Mwembemimba, Mwembetanga, Mwembenjugu, Mwembebeni, Mwembemakumbi, Mwembedezo, Mwembemchomeke na Kiembesamaki.

Miembeni

Miembeni ni mtaa uliopo baina ya *Mwembeshauri* kaskazini, *Mwembemadema* magharibi, *Kwaalinatu* mashariki na kusini upo jirani na *Kilimani*. Ni sehemu iliyokuwa na miembe mingi hapo zamani. Watoto wengi walikuwa na kawaida ya

kurandaranda chini ya miembe nyakati nyingi kwa ajili ya kuokota maembe. Mita mingi iliyopo jirani na Miembeni imeanza majina yake kwa neno la Mwembe kamavile *Mwembeshauri*, *Mwemberikunda*, *Mwembekisonge* na *Mwembemadema*. Hii inadhahirisha kuwa ardhi iliyopo sehemu hyo ni nzuri kwa kilimo hasa cha miembe licha ya kwamba miembe mingi imeshakatwa sasa kwa ajili ya kujenga nyumba za makaazi.

Mwembeshauri

Shauri ni kitendo cha kutoa wazo la kumsaidia mwengine (BAKIZA, 2010). *Mwembeshauri* ni mtaa uliyopo baina ya *Kariakoo* kwa upande wa mashariki, *Miembeni*, kusini, *Mwemberikunda* magharibi na upande wa kaskazini upo jirani na *Mwembekisonge*. Wakati wa harakati za kudai uhuru Waafrika wengi waishio Mjini na Vijijini walikuwa wanakuja sehemu hiyo kwa ajili ya kushauriana na kujadili mambo yao kisiasa na kijamii. Hivyo, watu walikuwa wanakwenda hapo chini ya mti wakisema, tunakwenda mwembeshauri.

Mwembemadema

Dema ni mtego wa kuvulia samaki unaotengenezwa kwa mwanzi, matete au vijiti (Bakhressa, 1999). *Mwembemadema* ni mtaa uliyopo jirani na *Miembeni* kwa upande wa kaskazini, *Maisara* magharibi, *Kariakoo*, mashariki na *Kilimani* kwa upande wa kusini. Hapo zamani, wavuvi walikuwa wanakwenda kuvua pwani ya Kizingo kwa kupitia *Maisara* kisha wanakutana chini ya muembe kwa ajili ya kutengeneza na kuyahifadhi madema yao ya kuvulia samaki, watu wakawa wanasema tunakwenda hapo Mwembemadema.

Mwemberikunda

Mtaa huu upo baina ya *Mwembeshauri* kwa upande wa kaskazini, *Miembeni* kusini, na *Michenzani* kwa upande wa magharibi. Amesimulia bw. Abdalla Mwinyi (Mkuu wa Mkoa wa Mjini 2014). Hapo zamani, mtaa wa *Mwemberikunda* kulikuwa na pirikapirika nyingi siku ya Jumamosi na Jumapili, kwa sherehe na ngoma asilia, kama vile benbati, sindimba, ngoma ya kibisa na manyago na fensi.

Mbele ya mwembe alikuwapo bwana mmoja anayeitwa Rikumba, mwenye asili ya Tanzania bara aliyekuwa mashuhuri sana kwa kazi yake ya kutengeneza viwinda na pingu wanazovaa wakwezi, wakati wa kukwea minazi. Hivyo, jina la mtaa huu limetokana na jina la mtu aliyekuwa akiishi katika eneo hilo la muembe.

Mwembeladu

Mdee na wenzake (2014), wameeleza kuwa ladu ni andazi gumu lenye umbo la mviringo na lenye ladha maalumu, linalotengenezwa kwa kutumia unga wa nafaka, kama vile mahindi au mtama, uliyochanganywa na viungo kama sukari, ufuta, tangawizi na asali. *Mwembeladu* ni mtaa uliyopo katika Wilaya ya Mjini, unapakana na *Kijangwani* kwa upande wa kusini, *Mitiulaya* kwa upande wa kaskazini, *Mwembemimba* upande wa mashariki na Magharibi upo jirani na *Kwabiziredi*. *Mwembeladu* hapo zamani kabla ya mapinduzi palikuwa pana mwembe pahala hapo, watu wengi walikaa sehemu hiyo kwa mazungumzo na kusubiri gari za kuendea shamba. Vile vile walikuwapo wanawake wa Kimanyema wakiuza ladu na togwa chini ya mwembe huo. Hivyo, kitendo cha kuuza ladu chini ya mwembe, kilisababisha jina la *Mwembeladu*.

Mwembemimba

Mimba ni utungo wa kiumbe katika tumbo la mwanamke kuanzia mbegu ya uzazi ya kiumbe inapoungana na yai la kike hadi kiumbe kuzaliwa (Mdee, 2014). *Mwembemimba* ni mtaa uliyopo baina ya *mwembeladu* kaskazini, *Mikunguni*, mashariki, na *Kijangwani*, kwa upande wa kusini. Amesimulia Bw Mohd Ali (mstaafu Habari / Maelezo, 2015), kuwa zamani gari za shamba zikiishia *Mwembemimba*, hivyo watu wote wakishuka hapo kisha wanatawanyika maeneo mengine. Wajawazito, wakiwekwa hapo chini ya mwembe kusubiri gari ya wagonjwa ya kuwapeleka Hospitali ya Mnazimmoja kwa ajili ya kujifungua. Siku moja alipita mke wa Gavana wa Uingereza aliyeitwa Father Wigo. Bibi huyu aliwaona wajawazito wengi waliokaa chini ya mwembe. Hivyo, alimuwarifu mumewe aliyekuwapo Uingereza na kuleta pesa zilizosaidia kujenga hospitali ya wazazi ya *Mwembeladu*. Kitendo cha wajawazito kukaa wengi chini ya mwembe huo, kilisababisha kupatikana kwa jina la *Mwembemimba*.

Mwembetanga

TUKI (1981), Tanga ni kitambaa kikubwa kinachofungwa kwenye mlingoti wa jahazi au mashua, ambacho hukinga upepo wenye kukisukuma chombo kiende mbele. Amesimulia Bi. Kauthari (Afisa Ukaguzi, 2014), mwanzoni kabisa mtaa huo ukiitwa kwa Bi Jokha, alikuwa ni mwanamke maarufu kwa ngoma ya kibuki (ngoma ya mashetani). Baadaye, jina hilo lilibadilika na kuitwa *Mwembetanga*. *Mwembetanga* ni mtaa uliyopo baina ya Vikokotoni kwa upande wa magharibi, Mtendeni, kaskazini, Michenzani, kusini na mashariki, upo karibu na Mapembeani ambako pia ni sehemu ya *Mwembetanga*. Chanzo cha mtaa huo, kupa wa jina hilo, ni

kuwa wavuvi, walikuwa wanakutana chini ya mwembe, ambapo ni masafa machache kutoka pwani ya Darajani kabla haijafukiwa, Wavuvi wakawa wanashona matanga kwa ajili ya mashua na jahazi zao.

Mwembenjugu

Njugu ni mbegu ya njugu yenye umbo dogo. Gamba gumu ambalo huota chini ya mzizi na hutumika kutengenezea mafuta ya karanga (TUKI 2014). Mwembenjugu ni mtaa uliyopo jirani na Mwembebeni kaskazini, Sogea kwa upande wa mashariki, Kwahani, magharibi na Kidongo chekundu, kusini. Katikati ya mtaa huo pana mzunguko wa barabara (round about) iliyougawa mitaa hiyo, katikati ya mzunguko huo kuna mwembe mkubwa, ambao hapo zamani, watu walikaa kuuza njugu.

Mwembebeni

Beni ni ngoma kubwa, pana iliyoambwa pande zote mbili, hupigwa upande mmoja kwa rungu na upande wa pili kwa mkono, aghalabu ngoma hii hupigwa kwa sherehe za harusi, hucheza kwa kuzunguka (BAKIZA, 2010). Mwembebeni ni mtaa uliyo jirani na Mikunguni kaskazini, Kibandamaiti mashariki, Mwembenjugu kusini na mashariki upo jirani na Kwaalimsha. Ni sehemu iliyokuwa ikifanywa mazoezi ya beni (mbwa kachoka) hapo zamani na ndipo walipokuwapo wapigaji beni mashuhuri kama vile wema na wenzake kutokana na mazoezi hayo yakifanyika chini ya mwembe, ndipo lilipoanza jina la Mwembebeni.

Mwembematarumbeta

Mdee na wenzake (2014), wamefafanua kuwa tarumbeta ni ala ya muziki ya kupuliza ambayo hutengenezwa kwa shaba na hutoa sauti kwa kubonyezwa vali

zake. Mwembematarumbeta ni mtaa uliyopo baina ya Jangombe, Kwahani na Kidongochekundu. Zamani kulikuwa na muembe mdogo pembeni mwa waya wa polisi, askari wanaoishi Bomani, walikuwa wakifanya mazoezi ya kupiga tarumbeta na bendi ya polisi, chini ya mwembe huo. Ndipo, watu wakapaita Mwembematarumbeta, ingawa sasa panaitwa Matarumbeta tu.

Mwembemakumbi

Kwamujibu wa Mdee na wenzake (2014), wamesema kuwa kumbi ni gome la nazi lenye nyuzinyuzi nyingi, ambazo hutumika kutengenezea kamba. Mtaa wa Mwembemakumbi upo baina ya Amani, Kilima hewa na Chumbuni. Jina jengine la mtaa huu ni Masumbani pahala ambapo pana kilima kikubwa kilichotokana na takataka za usumba. Amesimulia Bw. Haji Gora (mshairi mashuhuri, 2014) kuwa alikuwapo muhindi aliyeitwa Fadhil Shamsu, alikuwa na gari kubwa, aliyoitumia kukusanyia makumbi, kutoka pande zote za Kisiwa cha Unguja na kuyaweka chini ya mwembe, kisha yanafukiwa kwa ajili ya kutengenezea kamba zinazotumika kutengenezea vitanda, na mikoba.

Mwembemchomeke

Kuchomeka ni kitendo cha kutia kitu ndani ya kitu kingine (TUKI, 2010). Amesimulia Bw. Haji Pegwa (mwalimu, 2015) kuwa Mwembemchomeke ni pahala ambapo palikuwa na mwembe mkubwa walipopita wanawake nyakati za usiku walibakwa, kuporwa mali zao na kutishiwa amani. Hivyo, kutokana na vitendo hivyo, watu walijenga khofu na walipopita hapo, walisema hapa ndipo Mwembemchomeke.

Mwembedezo

BAKIZA (2010), dezo ni kupata kitu bila ya kutozwa gharama au kupata kwa bei ndogo. Mwembedezo ni, mtaa uliyopo karibu na Mwanakwerekwe, watu wengi hukaa hapo chini ya mwembe kwa kusubiri usafiri kama vile gari, au vespa kwa msaada, hivyo watu husema ninakwenda muembe dezo, kusubiri usafiri wa bure.

Kiembesamaki

Mtaa wa Kiembesamaki upo jirani na Uwanja wa ndege, kwa upande wa Kusini, Mbuyumnene Mashariki, Mombasa kaskazini na Mazizini kwa upande wa magharibi. Huu ni mtaa ulioanza zamani kabla ya Mapinduzi, wavuvi walikuwa wakikaa chini ya mwembe mdogo wanapotoka pwani kuvua na hukaa hapo, kuuza samaki. Wachuuzi wa samaki huwa wanakwenda hapo kwa ajili ya kununua samaki, nao husema, ” tunakwenda hapo Kiembesamaki”.

4.2.1.3 Mitaa Inayotokana na Mbuyu

Mbuyu ni mti mkubwa wenye kivimbakinene unaozaa matunda yenye gambagumu na kokwa nyingi. (BAKIZA, 2010) Pacha ni watoto waliozaliwa na mama mmoja kwa wakati mmoja. *Mbuyupacha* ni mtaa uliyopo jirani na *Kundemba* kwa upande wa Magharibi, *Kwahajitumbo*, Kaskazini, *Mfereji wa kiambazani*, Mashariki na *Mfereji Maringo* Kusini. Ni eneo lililokuwa na mibuyu miwili mikubwa iliyoshikamana.

Mbuyu kidambwita

Ni mtaa uliyopo jirani na *Misufini*, *Kundemba* na *Rahaleo* ni sehemu yenye mbuyu mfupi uliotandawaa matawi yake na kutoa kivuli kizuri, kwa wakaazi wa eneo hilo

wana kawaida ya kukaa chini ya mbuyu kwa ajili ya mazungumzo. Husema, “tupo hapa Mbuyu kidambwita” Kutokana na kivuli na upepo mzuri wanaoupata hapo.

Mbuyutaifa

Mbuyutaifa, upo jirani na *Gulioni*, *Mfenesimazizi*, *Mlandege* na *Kinazini*. Amesema TUKI (2004), taifa ni jumuiya ya watu wenye historia moja, utaifa mmoja na mfumo wa uchumi na siasa chini ya utawala mmoja. Mbuyutaifa, ni jina lililoibuka baada ya Mapinduzi ya Zanzibar 1964, viongozi walikuwa wanahimiza watu kushikamana na kuwa taifa moja lenye kufuata siasa ya ujamaa na kujitegemea. Raisi wa kwanza marehemu sheikh Abeid Amaan Karume aliwataka Waafrika waungane ili wawe taifa moja na kuondoa ubaguzi wa aina zote. Hivyo, watu walikuwa wakikutana chini ya mbuyu kwa mazungumzo wakati wa jioni makabila kama vile Wahindi, Waarabu na Waafrika, wakijadili mambo mbalimbali ya kuleta maendeleo katika nchi yao bila ya ubaguzi wowote.

4.2.1.4 Miti Mingineyo

Mtendeni

Mtende ni mti mnene unaofanana na mkindu, unaozaa matunda manjano, matamu yanapoiva. (2010, BAKIZA) Mtendeni ni mtaa uliyopo baina ya *Mwembetanga*, *Mchangani*, *Vikokotoni* na *Darajani*. *Mtendeni* ni mtaa uliyokuwa na mtende mkubwa hapo zamani, watu walikuwa na kawaida ya kukaa chini ya mtendeni, kuzungumza, ndipo lilipopatikana jina la *Mtendeni*.

Mkunazini

Mkunazi ni mti mkubwa wenye majani madogo madogo ya duara unaozaa matunda madogo madogo ya mviringo yenye ukaafu au ukakasi yakiiva ni matamu (TUKI,

2004). *Mkunazini* ni mtaa uliyopo katika eneo la *Mji mkongwe* tangu miaka mingi ya nyuma. Mapisi yatueleza kuwa ndipo, palipokuwa na soko la watumwa kwa wakati huo. Hapo zamani, palikuwa na miti mingi ya mikunazi katika eneo hilo ndiyo sababu, pakaitwa *Mkunazini*.

Mlandege

BAKIZA (2010), wameeleza kuwa, mlandege ni mti unaoota kwenye miti mingine, matunda yake mabivu, hupendwa sana kuliwa na ndege. Mlandege ni mtaa uliyopo jirani na *Gulioni* kwa upande wa Kaskazini, *Kwahajitumbo* Mashariki, *Msufini* Kusini na Magharibi upo jirani na *Mchangani*. Amesimulia Bw. Hassan Igumba (mkaazi, Mlandege, 2015) kuwa zamani ulikuwapo mti uitwao mlandege nyuma ya kituo cha polisi, ndege wengi walikuwa wakija pahala hapo wakati wote kwa ajili ya kula matunda ya mti huo. Chini ya mti huo alikuwapo mtu aliyekuwa na kawaida ya kuwapiga ndege kwa panda kisha aliwachoma na kuwala. Watoto nao, walipenda sana kucheza sehemu hiyo na kutega ndege kwa urimbo kisha waliwafugia kwenye tundu la ndege. Watu walikuwa walipowatafuta watoto wao waliambiwa wako kwa mlandege ndipo lilipozoeleka jina la *Mlandege*.

Mikunguni

Mdee na wenzake (2014), walieleza kuwa, mkungu ni mti unaozaa matunda yenye kokwa na badamu ndani ya hiyo kokwa, ambao ganda lake na hiyo badamu, vyote huliwa. *Mikunguni* ni mtaa uliyopo jirani na *Mkele*, kwa upande wa Kaskazini, *Amani* kwa upande wa Mashariki, *Kibandamaiti* Kusini na Magharibi, imepakana na *Kwaalimsha*. Bw. Murshid Rashid, (mkaazi, Mikunguni, 2015) kuwa, historia ya jina la *Mikungun*, imeanza mbali sana. Hapo kabla ya jina hilo kulikuwa na mti

mkubwa wa Mkungu, mti huo ulikuwa na kivuli. Watu waliokuwa wakenda mazikoni Kibandamaiti, kwa ajili ya kuosha maiti yao na kuzikwa *Makaburimswafa* walipumzika kidogo, chini ya mkungu huo. Mkungu huo ulikuwapo nje kidogo ya ukuta wa *Skuli ya Mikunguni*. Kutokana na umaarufu wa mti huo, mtaa wote ulijulikana kwa jina la *Mkunguni*. Mikungu iliendelea kupandwa kwa wingi kuelekea bondeni mwa barabara ya *Mikunguni*. Jina likabadilika na kuwa Mikunguni.

Kikwajuni

Mkwaju ni mti unaozaa matunda marefu yenye ugwadu (ukali) yatumikayo kuwa, kiungo cha mchuzi na kinywaji (TUKI, 1981). *Kikwajuni* ni mtaa uliyopo baina ya *Kisiwandui*, kwa upande wa Kaskazini, *Gongoni*, Mashariki, *Maisara* Kusini na Magharibi, imepakana na *Mnazimmoja*, pahala ambapo palikuwa na bahari, baadaye pakafukiwa na kujengwa majengo ya *Mnazi mmoja* na *Darajani*. *Kikwajuni* ni mtaa ulioanza zamani tokea wakati wa Mjerumani. Chanzo cha kupawa jina la *Kikwajuni* palikuwa na mkwaju uliyodumaa. Mkwaju huo, ndiyo uliyotoa miti mingine mingi baadaye.

Migombani

Mgomba ni mmea wa kiasi wenye kigogo laini chenye tabaka na majani marefu mapana unaozaa ndizi (BAKIZA, 2010). *Migombani* ni mtaa uliopo Ngambu jirani na Jangombe, Kilimani, Urusi na Kaburikikombe. Zamani lilikuwa ni shamba kubwa la migomba iliyoenea sehemu kubwa na zikioteshwa ndizi kamavile pukusa, mjenga, koroboi na mzuzu. Ndipo lilipoanzishwa, jina hilo, baadaye migomba ilikatwa na kuanzishwa majengo ya makaazi.

Michenzani

Mchenza ni mti wa jamii ya mchungwa unaozaa matunda matamu ya rangi ya kijani na yenye utufjuu (Bakhressa, 1999). Michenzani ni mtaa uliopo katikati ya mji ulioanza baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964. Marehemu Mzee Abeid Amaan Karume alianzisha majengo ya makaazi ya wananchi ambayo ni ya ghorofa. Kabla ya majengo hayo kujengwa palikuwa na miti mingi ya michenza katika eneo hilo. Baadaye ilikatwa na kujengwa majengo hayo lakini jina lilibakia lilelile la awali la Michenzani. Mtaa wa Michenzani umepakana na mitaa mingi kamavile Mlandege, Rahaleo, Mwembeshauri, Miembeni, Maisara. Kikwajuni, Vikokotoni na Mwembetanga, katikati ya Michenzani pana Bwawa kubwa la maji lililokuwa likitoa mandhari nzuri ya rangi tafauti hapo zamani.

Mkungumalofa

Ni mtaa uliopo baina ya Mwembeshauri, Miembeni, na Kariakoo. Hapo zamani palikuwa na mkungu mkubwa uliotawanya matawi yake na kutoa kivuli kizuri. Watu wengi wakipendelea kukaa sehemu hiyo kwa ajili ya mazungumzo, wengi wao walikuwa masikini wasiokazi ya kufanya hutumia muda wao mwingi kwa mazungumzo na kuomba kwa wapiti njia.

4.2.2 Majina Yenye Asili ya Watu

Majina yenye asili ya watu haya ni majina yaliyopatikana kutokana na watu mashuhuri

Jedwali Na 4.2: Majina Yenye Asili ya Watu

Na.	Mtaa	Jina la Mtu
1.	Kwahani	Ali Hani
2.	Kwaalinatoo	Ali Natoo
3.	Kwaalimsha	Ali Mcha
4.	Kwahajitumbo	Haji
5.	Kwamtipura	Mohammed Mtiptip
6.	Kwabiziredi	Ziredi
7.	Kwasharifumsaa	Sharifu Mussa
8.	Amani	Amani
9.	Lumumba	Patric Lumumba
10.	Nyerere	Julius Kambarage Nyerere

Chanzo: Mtafiti (2014)

4.2.2.1 Majina yenye Asili ya Watu

Haya ni majina ya mitaa yanayotokana na watu mashuhuri ambao ni vigumu kuwasahau. Uteuzi wa jina la mtu ambalo hutumika katika mitaa hutegemea umashuhuri, umaarufu au alikuwa wa kwanza kuhamia eneo hilo. Majina yenye asili ya watu yanayopatikana Mjini Unguja ni kamavile *Kwahani*, *Kwaalinatoo*, *Kwahajitumbo*, *Kwamtipura*, *Kwabiziredi*, *Nyerere*, *Amani*, *Lumumba*. *Maisara* na *Kwaalimsha*.

Kwahani

Kwahani ni mtaa uliopo jirani na Kwaalimsha kwa upande wa Kaskazini, Kidongo chekundu, Mashariki, Matarumbeta Kusini na upande wa Magharibi imepakana na Kwaalinatu. Mtaa wa Kwahani umepata jina kutokana na mtu mashuhuri aliyekuwa akimiliki eneo hilo aliyetitwa Ali Hani. Amesimulia Mzee Nassir (sheha wa Kwahani, 2014) kuwa, mmiliki wa eneo hilo, Ali Hani, mwenye asili ya kihindi, alimiliki shamba kubwa, alijenga nyumba na msikiti uliokuwa na kisima mbele yake

ambao upo hadi sasa. Alijenga maghala mawili makumbwa yaliyotumika kuhifadhiya bidhaa kama nazi na karafuu, wachukuzi wa bidhaa hizo walikuwa ni askari wakiitwa carries crops kutokana na watu kushindwa kutamka neno hilo wakawa wanasema kariakoo ndipo lilipopatikana jina la Kariakoo, mtaa ambao upo masafa machache kutoka Kwahani.

Kaskazini ya Kwahani kuna uwanja mkubwa unaoitwa uwanja wa farasi, watu kutoka majumba ya mawe wakija katika eneo hilo kwa ajili ya kufanya mashindano ya mbio za farasi, lilikuwa eneo lenye mandhari nzuri ya kuvutia, vilijengwa vibaraza vya kukaa waangaliaji na njia za kukimbilia farasi lakini kwa sasa ni uwanja wa kuzalishia mbu. Wakaazi waliyokuwa wakiishi Kwahani walilazimika kulipa pesa mbili kwa kila nyumba ikiwa ni kodi ya shamba la Bw. Ali Hani. Kutokana na umaarufu wa Ali Hani ndipo lilipopatikana jina la Kwahani.

Kwaalinatedu

Kwaalinatedu ni mtaa uliopo mkabala na Kariakoo, Kwahani na Miembeni. Hapo zamani kabla ya Mapinduzi alikuwapo mtu mashuhuri akishona viatu, mikoba na miamvuli iliyochanika, akiitwa Ali Natoo. Hivyo watu walikuwa na kawaida ya kupeleka viatu vyao kushonwa na wakisema “Peleka hapo Kwaalinatedu viatu vyako akushonee. Ndipo lilipopatikana jina hilo.

Kwahajitumbo

Ni mtaa uliyopo baina ya *Mlandege*, *Gulioni*, *Kwabiziredi* na *Mbuyupacha*. *Kwahajitumbo* ni mtaa uliyopata jina kutokana na mtu mashuhuri aliyeitwa Haji alikuwa na tumbo kubwa, alikuwa ana kawaida ya kukaa sokoni akiuza kitoweleo.

Hivyo, watu wakipita walikuwa wakimwita Haji tumbo na wengine majumbani, wakiwatuma watoto wao kitoweleo wanawambia “nenda kwa Hajitumbo kununua kitoweo”. Ndipo lilipopatikana jina hilo.

Kwabiziredi

Kwabiziredi ni mtaa uliopo baina ya Mwembeladu, Rahaleo, Mbuyupacha na Gulioni. Eneo hilo zamani lilikuwa ni shamba lililomilikiwa na mwanamke aitwae Ziredi. Alijenga nyumba, msikiti na mbele ya msikiti ndipo walipokuwa wakizikana, mmoja wa familia anapofariki. Kutokana na umaarufu wa mwanamke huyu ndipo lilipopatiakana jina la Kwabiziredi.

Nyerere

Nyerere ni mtaa uliyo jirani na *Kibandamaiti, Sogea, Begamoja na Sebleni*. Mtaa huu umepata jina hilo baada ya Mapinduzi ya Zanzibar 1964 na Uhuru wa Tanganyika 1961 ulifanyika Muungani wa Tanganyika na Zanzibar na kupatikana Tanzania. Nyerere ni jina la Raisi wa kwanza wa Tanzania Mw. Julius Kambarage Nyerere ikiwa ni ukumbusho na heshima.

Kwamtipura

Kwamtipura ni mtaa uliyopo baina ya *Amani, Kilimahewa, Chumbuni na Mwembemakumbi*. *Kwamtipura* ni mtaa ulioanza miaka mingi ya nyuma. Amesimulia bi, Nuru (mkaazi, Kwamtipura, 2015) kuwa Kwamtipura zamani lilikuwa, shamba kubwa, lililokuwa na miti mingi kama vile miembe, miwa na mipera. Miaka mingi iliyopita walikuja wafanyabiashara kutoka nchi za nje, miongoni mwao ni mfanyabiashara mashuhuri aliyetitwa Mohamed Ahmed Marjesh

jina la umaarufu akiitwa Tiptip. Akifanya biashara ya utumwa, ndovu na dhahabu alipokuja Zanzibar alifikia eneo hilo, watu wakipaita Kwamtiptip baadaye pakaitwa Kwamtipura.

4.2.3 Majina Yaliyotokana na Mazingira

Haya ni majina yaliyotokana na hali ya maumbile ya eneo husika

Jedwali Na 4.3: Majina ya Mazingira

Na	Mtaa	Maumbile
1.	Kidongochekundu	Sehemu yenye udongo mwekundu
2.	Kilimahewa	Sehemu ya Kilima yenye hewa safi
3.	Kilimani	Sehemu iliyo juu
4.	Kijangwani	Sehemu isiyoota miti (jangwa)
5.	Kijito upele	Sehemu yenye mto wa maji
6.	Mtoni	Sehemu yenye mto wa maji
7.	Vikokotoni	Sehemu yenye vikokoto vya mawe
8.	Mchangani	Sehemu yenye mchanga mwingi
9.	Darajani	Sehemu yenye daraja la kuvukia
10.	Daraja bovu	Sehemu yenye daraja bovu

Chanzo: Mtafiti (2014)

4.2.3.1 Majina ya Mazingira

Kidongochekundu

BAKIZA (2010), wameeleza kuwa kidongo ni udongomwekundu unaotumika kufanyia vitu kama vile vyungu, vyetezo, mikungu na mitungi. *Kidongochekundu* ni mtaa uliopo baina ya *Jangombe, Urusi, Meya na Magomeni*, umepewa jina hilo kutokana na udongo wa sehemu hiyo kuwa mwekundu.

Kilimahewa

Ni mtaa uliyopo baina ya *Kwamtipura, Amani, Chumbuni na Mwembemakumbi* ni sehemu yenye kilima kirefu chenye hewa safi, nyumba za wakaazi ziko juu ya kilima hivyo wanapata upepo mzuri katika eneo hilo.

Kijangwani

Kijangwa ni sehemu isiyoota miti. *Kijangwani* ni mtaa uliyo jirani na *Kariakoo* Kusini, *Rahaleo* Magharibi, *Mwembeladu* Kaskazini na *Kwaalimsha* Mashariki. Eneo hilo hapo zamani lilikuwa ni jagwa hakuna miti wala majumba lakini kutokana na kukua kwa mji sasa pana majumba mengi na pia, upo uwanja wa mpira uitwao Kombawapya lenye maana, wageni wengi waliohamia.

Mtoni

Mdee na wenzake (2014) wameeleza kuwa mto ni korongo ambalo huwa na maji yanayotiririka karibu wakati wote wa mwaka, kutoka kwenye mwinuko kwendea bondeni. Mtoni ni mtaa uliyopo baina ya Beit el ras, Maruhubi na Mwembemakumbi, ni mtaa ulioanza miaka mingi iliyopita tokea enzi ya utawala wa Sultani, palikuwa pana jumba kongwe la kifalme lililoitwa Beit el Mtoni. Jumba hilo lilikuwa karibu ya pwani lililozungukwa na miti ya kila aina inayoota katika nchi za joto. Jina la mtoni lilipewa jumba hilo kutokana na mto mdogo utokao upande wa ndani wa kisiwa, na kwa masafa mafupi baadae yakilipita jumba hilo umefanya mahali pa kumwagia maji yake na kuingia baharini. Jina la Beit el mtoni baadaye lilikufa na mtaa wote ukabakia na jina la Mtoni.

Kilimani

Kilimani ni mtaa ulio jirani na *Migombani*, *Maisara*, *Miembeni* na Kusini umepakana na bahari ya Hindi. Mtaa huu umepewa jina hilo kutokana na muinuko mkubwa uliyopo hapo. Zipo nyumba za maendeleo za roshani zilizojengwa baada ya Mapinduzi ya Zanzibar 1964, ambazo ziko juu ya kilima ni pahala penye mandhari ya kuvutia, upepo mwanana unaoelekea pwani unaowaburudisha wakaazi.

Kijitoupele

Upele ni uvimbe mdogo mdogo ulioenea mwilini na aghalabu huwasha na kutoa usaha (Bakhressa, 1999). Mtaa wa Kijitoupele uko jirani na *Mwwnakwererekwe, Fuoni na Nyarugusu* ni sehemu yenye mto uliojengewa kidaraja cha kupitia watu. Hapo zamani palitokea maradhi ya upele yaliyowaathiri watoto wengi, wazazi walikuwa wanawapeleka watoto wao hapo, kwa kuwaosha na kuwasugua kwa mchanga wa mtoni, na watoto walikuwa wanapowa. Hivyo, watu wakapaita *Kijitoupele*.

Vikokotoni

Mdee na wenzake (2010), wamesema kokoto ni mawe yaliyopasuliwa vipande vidogo vidogo lakini vikubwa kuliko changarawe kwa ajili ya kujengea. Mtaa wa Vikokotoni unapakana na Darajani Kaskazini, Mwembetanga Mashariki, Michenzani Kusini. Hapo zamani mji ukijengwa majengo ya kuishi watu. Walikuwapo watu wenye asili ya kihindi wakifanya kazi ya kuchukua mawe sehemu za shamba kwa nyumbu na punda kisha huyaleta hapo kwa ajili ya kuyavunja kokoto na kuziuzwa. Watu wengi walikwenda kununua kokoto za ujenzi, baadaye walipaita pahala hapo Vikokotoni.

4.2.4 Majina ya Matukio

Haya ni majina ya mitaa yaliyotokana na matukio ya kihistoria yaliyotokea hapo zamani Mjini Unguja ambayo athari yake imebaki hadi leo.

Jedwali Na 4.4: Majina ya Matukio

Na.	Mtaa	Tukio
1.	Kisiwandui	Pakiwekwa wagonjwa wenye maradhi ya ndui
2.	Kibandamaiti	Kibanda cha kukoshea maiti
3.	Rahaleo	Majengo ya kisasa
4.	Kajificheni	Mkaliano wa majengo
5.	Mchambawima	Kukoga hadharani
6.	Shaurimoyo	Tabia mbaya za wenyeji
7.	Mpendae	Harusi nyingi
8.	Begamoja	Kukaribia masafa
9.	Gulioni	Soko la kuuzia bidhaa
10.	Makadara	Makadirio ya Mungu
11.	Ziwatuwe	Watu watulize roho zao
12.	Kudemba	Burudani za kila aina
13.	Kariakoo	Askari waitwao carries crops
14.	Mfereji maringo	Mfereji utokao maji kidogo kidogo
15.	Jang'ombe	Tabia kama za wanyama
16.	Kaburi kikombe	Kaburi la biharusi
17.	Mgeni haji	Kutokupokelewa vizuri
18.	Mwanakwerekwe	Maji mengi
19.	Bububu	Mlio wa reli
20.	<i>Kisimamajongoo</i>	Kisima chenye majongoo
21.	<i>Saateni</i>	Miadi ya kukutana saa mbili

Chanzo: Mtafiti (2014)

4.2.4.1 Majina ya Matukio

Haya ni majina ya mitaa yaliyotokana na matukio ya kihistoria yaliyotokea hapo zamani Mjini Unguja ambayo athari yake imeweka kumbukumbu hadi leo. Majina hayo ni *Kisiwandui*, *Kibandamaiti*, *Mchambawima*, *Shaurimoyo*, *Gulioni*, *Makadara*, *Kudemba*, *Jangombe Kaburikikombe* na *Mpendae*

Kisiwandui

TUKI (2004), wamesema kisiwa ni fungu la nchi kavu lililozungukwa na maji pande zote. Ndui ni ugonjwa wa ngozi unaoambukiza unaoacha alama mwilini unafanana na tetekuwanga. Kisiwandui ni mtaa uliopo baina ya *Vikokotoni, Kikwajuni na Gongoni*.

Amesimulia bi. Zulekha Kombo (Mkurugenzi Utalii, 2015) kuwa hapo zamani eneo la *Kisiwandui* lilikuwa kisiwa kilichozungukwa na maji katika miaka ya 1800 ulizuka ugonjwa wa ndui, ulikuwa ugonjwa wa kuambukiza, hivyo watu walitengwa ili wasije wakawaambukiza wengine kwa kuwekwa kisiwani ili wasichanganyike na watu wengine. *Darajani* palikuwa na daraja la kuvukia bahari kwendea *Mji mkongwe*. Baadaye Serikali ya Kikoloni ilifukia bahari yote ya *Mji mkongwe* na kuwa sehemu ya nchi kavu yenye majengo mengi.

Kibandamaiti

Kibanda ni kijumba kidogo kinachotumika kwa shughuli maalumu. Maiti ni mwili wa mtu aliyekufa (TUKI, 2004). *Kibandamaiti* ni mtaa uliyopo baina ya *Mikunguni Amani, Nyerere na Begamoja*. Zamani kabla ya Mapinduzi watu waliofariki waliyotoka Mjini walikuwa wakipelekwa *Kibanda maiti* pahala ambapo paliwekwa maalumu kwa ajili ya kukosha maiti, na wapo watu maalumu wakiosha maiti, kisha maiti huyo alipelekwa Makaburi mswafa ambako kulichimbwa makaburi na askari maalumu na kuzikwa, pahala ambapo ni masafa machache kutoka Kibanda maiti. Mwanzo watu walizikwa *Ziwa tuwe* baadaye, Serikali ilitoa amrisha watu wazikwe *Kibandamaiti*, watu walioishi mitaa jirani na hapo walisema sasa tumepata nafuu

masafa yamepungua tutazikana hapo begamoja tu na sisi, ndipo lilipopatikana jina la mtaa wa *Begamoja*.

Shaurimoyo

Shauri ni hoja inayohitaji kujadiliwa, mawaidha, nasaha, maoni au elekeza (Mdee na wenzake, 2014). Shaurimoyo ni mtaa uliyopo baina ya Mkele, Saateni, Kwaabasiuseni na Mboriborini. Mtaa huu umepewa jina la Shaurimoyo kutokana na tabia mbaya walizonazo wakaazi wake.

Amesimulia Bw. Madai Jaffari (Mkaazi wa Shaurimoyo, 2015), kisa chake binafsi, kilichomfanya ahame Shaurimoyo kwenye nyumba yake na kuazimwa banda katika mtaa wa Mpendae kutokana na vituko vya mtaa huo, anasimulia kuwa watoto wake wamepigwa mapanga na kikundi kinachojiita ubayaubaya kinachoishi Shaurimoyo, majirani washirikina wanamfanyia kila aina ya vituko, watu wanachoyo wakimuona mtu ameingia na debe tupu la samli wanapiga mafumbo. Mwisho aliishia kwa kusema ushauri moyo wako kweli kabla hujahamia mtaa ule.

4.2.4.2 Mpendae

Ni mtaa uliyopo jirani na *Jangombe, Migomban na Mombasa*. Zamani katika eneo hilo lilikuwa pori kubwa lenye mikarafuu, mizambarau na mifuu, baadaye Serikali iligawa viwanja kwa ajili ya kujenga nyumba za makaazi. Watu wengi waliojenga walikuwa hawajaoa hivyo wanapohamia kwanza huoa, ikawa kila anayehamia ni bibi harusi au bwana harusi wakaazi wakawa wanatania kwa kusema huu mji wa wapendanao. Ndipo lilipopatrikana jina la Mpendae.

Gulioni

Gulio ni sehemu yenye soko la uwanjani linalofanywa kila baada ya muda maalumu (BAKIZA, 2010). Mtaa wa Gulioni kulikuwa na soko la wiki kila siku ya Jumapili paliuzwa bidhaa mbalimbali zinazotoka mjini, shamba na maeneo mengine. Watu wengi wakihudhuria hapo kwa ajili ya kupata mahitaji ya wiki, yakiwemo vyakula, nguo na bidhaa za nyumbani. Watu walikuwa wakihimizana kwa kusema “tusikose Gulioni wiki hii”. Ndipo lilipopatikana jina la hilo.

Makadara

Makadara ni mtaa uliyopo baina ya *Lumumba*, *Mikunguni*, *Mwembemimba* na *Mwembeladu*. Zamani maeneo haya yalikuwa hayaishi watu ni sehemu ya pori kubwa. Alikuwapo bwana mmoja aliyetitwa Marzuku Kombo akiishi *Mwembetanga* lakini aligombana na jirani zake na kuamua kuhama akajenga kibanda chake hapo msituni watu wakawa wakipita walimuuliza “Mzee marzuku mbona umehamia msituni peke yako?”

Akijibu “haya ndiyo makadara ya Mungu” akimaanisha kuwa Mungu ndivyo alivyompangia kuishi mwituni peke yake. Watu wa *Mwembetanga* baadhi yao wakawa wanaulizana Mzee Marzuku yuko wapi? Wanajibiwa yuko katika makadara yake, ndipo lilipopatikana jina la *Makadara*.

Kundemba

Ameeleza Bw. Abdalla Ali (2014), kuwa kundemba maana yake ni kustarehe. Mtaa wa Kundemba zamani ulikuwa ni mtaa wa starehe za kila aina, watu wakipitapita na kustarehea maisha. Utawaona watu wanaingia ndani ya vijumba wakiwa na akili

zilzotulia wakitoka chakari wameshalewa. Kundemba kulikuwa na vurugu za maisha na burudani. Palikuwa makao makuu ya mbwakachoka (beni) ngoma ambayo haihitaji mtu kufundishwa kucheza kwani haina utaratibu maalumu, kulipatikana tamasha na tafrija za usiku zilizokwenda sambamba na ngoma kama vile bom, lelemama, kunguwiya, kurusha vishada na tiyara. Mzee Mwi Mzee Mwinyi alikuwa bingwa wa kutengeneza vishada vya kila aina na kila rangi. Watoto na watu wazima wakipenda kurusha vishada vya Kundemba ili kupitisha muda wa kusubiri futari katika mwezi wa Ramadhani wakati waislamu wanapofanya ibada ya saumu (kufunga mwezi Mtukufu wa Ramadhani).

Mchambawima

Kuchamba ni kitendo cha kusafisha kwa maji sehemu za siri baada ya kwenda haja Wima maana yake simama au nyooka kuelekeawima (BAKIZA, 2010). Mchamba wima ni mtaa uliopo baina ya *Mkunazini, Kajificheni na Darajani*. Hapo zamani palikuwa ni sehemu ya kuchunguzwa maziwa yote yanayouzwa Mjini Unguja, wafanya biashara ya maziwa asubuhi mapema wanakuja hapo ili kuchunguzwa maziwa kama yako safi hayajatiwa maji, kisha wanapewa idhini ya kusambaza.

Siku moja alitokezea mwanamme mmoja aliyelala kwa mwanamke katika eneo hilo hadi asubuhi ikachomoza, mbele ya duka la mkaguzi wa maziwa pana mfereji. Hivyo, yule kijana alipoamka akajiona ameshachelewa alifadhaika na kutoka mbio kwenda kwenye mfereji kukoga bila ya kujua kuwa wauza maziwa wameshafika wanamuona. Wauza maziwa walipomuona walimjua kuwa huyo si mkaazi wa hapa na walifahamu kitendo alichokifanya wakawa wanaoneshana kwa kusema muangalie yule mchambawima ndipo lilipopatikana jina hilo.

Kaburi Kikombe

Ni mtaa uliopo baina baina ya Mpendae, Kilimani na Migombani, hapo zamani alikuwapo msichana ambae alikuwa akitarajiwa kuolewa siku ya Ijumaa. Ilipofika Alkhamis, jioni alifariki na kuzikwa siku ya Ijumaa. Siku ambayo ilitarajiwa kuwa ndio siku ya harusi yake, wazee wake waliamua azikwe juu ya kaburi lake palibandikwe vikombe kama ishara ya harusi yake, ndipo mtaa huo ukaitwa Kaburi kikombe.

Jangombe

Mtaa wa Jang'ombe ni mtaa maarufu sana katika Kisiwa cha Unguja. Mtaa huo ni miongoni mwa mitaa ya mwanzo iliyokuwa ikijulikana kama ng'ambu (si mjini wala si shamba). Mtaa huu upo baina ya Magresheni ya zamani, Ziwani polisi, Mpendae na Migombani. Asili ya jina hilo alikuwapo mzee aliyeishi Makunduchi, siku moja aliwatembelea jamaa zake wanaoishi Kilimani, wakati huo usafiri ulikuwa wa tabu sana kutoka Makunduchi hadi Mjini, hivyo alipata usafiri wa msaada hadi Fuoni ulikuwa usiku umeshaingia. Alitembea kwa miguu hadi Wayani na kufika Shule ya Jang'ombe saa nne usiku.

Hivyo, akatafuta huku na huku na kupata mti uliokuwa umelimiwa vizuri akalala. Kwa ufupi hakulala kwa mawazo na woga, asubuhi ilipofika alishukuru kwa kuamka salama alikwenda kwa jamaa zake na kuwasimulia mkasa uliyompata, alulizwa na mwenyeji wake. Hee mwenzetu msituni ulilalaje? Akasema nililala ja ng'ombe. Neno "Ja" kwa lahaja ya kimakunduchi ni sawa na kama akimaanisha amelala kama ng'ombe. Habari ya mzee huyo ilienea na tokea siku ile mtaa huo ukaitwa Jangombe.

Mwanakwerekwe

Mtaa wa Mwanakwerekwe upo baina ya Magomeni, Mombasa, Fuoni na Magogoni. Ni mtaa uliyoendelea zaidi katika miaka ya themanini wakati yalipojengwa majengo ya maonesho, watu wengi wakaanza kujenga majengo ya makaazi, lipo soko kubwa la bidhaa zinazouzwa kwa mnada, watu wengi hujaa wakati wa asubuhi kwa ajili ya kujipatia mahitaji muhimu. Pembeni mwa soko pana bwawa kubwa lililotokana na kuchimbwa mchanga, maji mengi yanakaa hapo. Hapo zamani Mwanakwerekwe, palikuwa ni sehemu yenye kukaa maji mengi siku za mvua, siku moja alipita mwanamke amemshika mkono mtoto wake na huku wanavutwa na maji, watu wakamwambia “Huyo mwana kwerekwe” yaani huyo mtoto mbebe. Kwerekwe ni lahaja ya watu wa kusini yenye maana ya mchukue au mbebe. Kutokana na kauli hiyo ndipo lilipopatikana jina la mtaa wa Mwanakwerekwe.

Kajificheni

Kajificheni ipo katika eneo la *Mji Mkongwe* baina ya *Mchambawima*, *Hamamni*, *Kiponda* na *Sokomuhogo*. Ni mtaa uliyoshikamana majengo yake watu wengi watokao Nga'mbo walikuwa wakipotea walipofika maeneo hayo kutokana na majengo yake yamefanana sana na yamekaliana watu wakawa wanasema” nendeni kajificheni”

Kisimamajongoo

Ni mtaa uliopo jirani na Gongoni, Kikwajuni na Michenzani. Hapo zamani palichimbwa kisima cha maji lakina bahati mbaya yakawa yanatoka majongoo mengi ndani ya kisima ndipo watu wakakiita kisima majongoo na baadaye mtaa wote ukapewa jina la Kisimamajongoo.

Mferejimaringo

Mtaa wa Mferejimaringo upo baina ya Kundemba upande wa Magharibi, Rahaleo Kusini, Kwabiziredi Mashariki na Kaskazini upo jirani na Mbuyupacha. Hapo zamani kabla ya Mapinduzi ya 1964, Huduma ya maji safi ilikuwa ina tabu kupatikana kwa wananchi hivyo, utawala wa wakati huo waliweka mifereji katika maeneo ya Mjini ili kuwapunguzia wananchi tatizo la maji. Ulikuwapo mfereji uliowekwa kwenye kiambaza cha nyumba pakawa panaitwa mfereji wa kiambazani, ulikuwepo mfereji uliowekwa ndani ya shimo ili maji yaweze kutoka kwa kasi pahala hapo palipewa jina la mfereji wa shimo. Mferejimaringo maji yake yalikuwa yanatoka kidogo kidogo kwa sababu ulikuwa mfereji wake upo juu, maji mengi yalikwenda mfereji wa shimo ndipo watu waliuita mferejimaringo na baadaye mitaa hiyo yote ikapewa majina hayo ya mifereji.

Bububu

Ni mtaa uliopewa jina lake kutokana na kuigizwa sauti ya reli iliyokuwa ikilia bu bu bu. Reli hii ilikuwa ikifanya safari zake kuanzia Bwawani, Kinazini, Maruhubi, Mtoni, Beit el ras na kumazia hapo Bububu kwa kupitia katika sehemu ya ufukweni mwa bahari katika miaka mingi iliyopita sasa yamebakia mabaki machache ya njia ya reli hiyo bahari.

Muungano

Mtaa wa Muungani upo baina ya Kidongochekundu, Magomeni na Sogea. Ni mtaa ulioibuka baada ya Uhuru wa Tanganyika na Zanzibar zikaunganishwa nchi hizi mbili na kupatikana Tanzania kwa vile fasihi ya majina inakwenda sambamba na jamii mtaa huu ukapewa jina la Muungano ili kuenzi Muungano huo.

Saateni

Ni mtaa uliopo jirani na Kinazini, Lumumba na Mtoni. Amesimulia Bw. Abdalla Juma(Mkaazi) kuwa hapo zamani alikuwepo mwarabu akiitwa Hamdani alikuwa anauza duka katika maeneo hayo, siku moja aliwekeana miadi na mwanamke aliyemtaka kimapenzi hivyo, mwarabu alikuwa na shauku kubwa ya kukutana na mwanamke huyo, akawa anakariri kila mara kwa kusema saatein saatein akimaanisha kuwa atakutana naye saa mbili. Watu waliosikia wakawa wanasema na wao saatein ndipo lilipopatika jina la Saateni.

Majina ya mitaa ya Unguja Mjini yana historia yake iliyohifadhiwa na jamii yake wenye kuelewa mambo yao ya kale yaliyoshikamana na fasihi yao. Daima huwezi kutenganisha fasihi na jamii kwani vinatembea sambamba na nadharia ya uhalisia imetumika kuongoza utafiti huu kwa kuchambua hali halisi ya Mji wa Unguja.

4.3 Kuchambua Vipengele vya Mtindo na Lugha

Haya ni madhumuni ya pili yaliyoongozwa na swali la pili lililouliza vipi vipengele vya mtindo na lugha vimejitokeza katika majina ya mitaa ya Mjini Unguja. Mtafiti alichambua vipengele vya fani kwa kuangalia mtindo na lugha iliyotumika kuundia majina ya mitaa. Mtafiti ametumia nadharia ya ndani nje katika kuchambua vipengele hivyo. Kwani uchambuzi wa mtindo na lugha iliyotumika katika majina ya mitaa sio rahisi kuiona kwa jicho la kawaida lazima uwe na darubini ya kuangalia ndani na nje ya majina hayo.

4.3.1 Maana ya Fani

Fani ni jumla ya mbinu, ufundi, usanii anaoutumia mwanafasihi katika kuwasilisha maudhui (Masebo, 2005). Hivyo, fani ni kiungo kikuu kinachowasilisha maudhui,

fani na maudhui ni sarafu moja yenye pande mbili. Miongoni mwa vipengele vinavyounda fani ni kama vile lugha, mtindo, muundo na mandhari. Lakini mtafiti katika kazi hii amechambua mtindo na lugha.

4.3.1 Mtindo

Mtindo ni jumla ya mbinu au sifa inayotumika ili kubainisha vionjo vya kazi ya fasihi (Senkoro, 2009), Mtindo hueleza jinsi kazi ya fasihi ilivyoundwa. Majina ya mitaa hayatolewi katika ombwe na si kweli kuwa hayana maana mahsusi kama baadhi ya watu na mitandao ya kijamii wanavyoeleza. Majina ya mitaa hutokana na miti, watu mashuhuri, mazingira na hata shughuli za kijamii. Hata hivyo, uundaji huu huzingatia mbinu maalumu kama vile mbinu ya mwambatano, eponimu, toponimu na mbinu ya usababishi na tokeo.

4.3.1.1 Mbinu ya Mwambatano

Hii ni mbinu ya kuunganisha maneno mawili au zaidi ili kuunda neno jipya (Mrikaria, 2004).

Jedwali Na 4.5: Mbinu ya Mwambatano

Na.	Jina la Mtaa	Shehia	Mbinu iliyotumika
1	<i>Mwembeladu</i>	<i>Mwembeladu</i>	Imetumika mbinu ya kuunganisha neno <i>Mwembe</i> na <i>Ladu</i> Pakiuzwa ladu chini ya mwembe huwo
2	<i>Mwembetanga</i>	<i>Vikokotoni</i>	<i>Mwembe</i> na <i>Tanga</i> Chini ya mwembe pakitengenezwa matanga ya wavuvi
3	<i>Miti ulaya</i>	<i>Makadara</i>	<i>Miti</i> na <i>Ulaya</i> Pameoteshwa miti mingi yenye asili ya Ulaya
4	<i>Mwembebeni</i>	<i>Muungano</i>	<i>Mwembe</i> na <i>Beni</i> Pakichezwa beni chini ya muembe
5	<i>Mwembedezo</i>	<i>Mwanakwerekwe</i>	<i>Mwembe</i> na (<i>Dezo</i>) bure Watu husimama kwa kusubiri msaada wa gari

Chanzo: Mtafiti (2014)

4.3.1.2 Mbinu ya Umashuhuri (Eponimu)

Hii ni mbinu ya uundaji wa maneno kwa kuzingatia mtu maalumu aliyevumbua au anayehusishwa na jambo fulani katika jamii. Dhana hii inaweza kupewa jina la heshima au kumbukumbu ya mtu mashuhuri. Mbinu ya eponimu hutumika zaidi katika uundaji wa majina ya mahali. (Gichuru, 2010) ameeleza kuwa mbinu hii ni maarufu katika kuundia majina ya barabara, mitaa, kampuni na taasisi.

Jedwali Na 4.6: Mbinu ya Umashuhuri (Eponimu)

Na.	Jina la Mtaa	Shehia	Kichocheo
1.	<i>Kwahani</i>	<i>Kwahani</i>	Jina la mwenye kumiliki shamba
2.	<i>Kwaalinatu</i>	<i>Kwaalinatu</i>	Mtu maarufu ambae ni mshoni wa viatu
3.	<i>Kwamtipura</i>	<i>Kwamtipura</i>	Mfanyabiasha wa mwanzo aliyehamia Zanzibar
4.	<i>Kwahajitumbo</i>	<i>Mlandege</i>	Mtu mashuhuri aliyekuwa na tumbo kubwa
5.	<i>Nyerere</i>	<i>Nyerere</i>	Raisi wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuonesha heshima na kumbukumbu

Chanzo: Mtafiti (2014)

4.3.1.3 Mbinu ya Kimazingira (Toponimu)

Hii ni mbinu ya kuunda majina ya mahali kutokana na hali fulani ya mazingira (Gichuru, 2010), mbinu hii huzingatia zaidi maumbile ya eneo husika. Hali hii inaonesha kuwa uundaji wa majina ya mitaa katika jamii ya waswahili hutegemea vitu wanavyovionika katika mazingira yao na majina hayo huwa ni rahisi kukubalika na wazungumzaji wa lugha hiyo.

Jedwali Na 4.7: Mbinu ya Kimazingira (Toponimu)

Na	Majina ya Mitaa	Shehia	Hali ya Mazingira
1.	<i>Kilimahewa</i>	<i>Amani</i>	Kuwapo kwa Mlima na hewa safi
2.	<i>Kijangwani</i>	<i>Mwembeladu</i>	Eneo la wazi ambalo halina miti
3.	<i>Kilimani</i>	<i>Kilimani</i>	Kuwapo kilima katika eneo hilo
4.	<i>Mtoni</i>	<i>Mtoni</i>	Kuwapo mto wa maji katika sehemu hiyo
5.	<i>Kidongochekundu</i>	<i>Kidongochekundu</i>	Kuwapo udongo mwekundu

Chanzo: Mtafiti (2014)

4.3.1.4 Mbinu ya Usababishi na Tukio

Hii ni mbinu ambayo matukio yanafuatana kwa mpangilio wa kimuundo unaoonesha uhusiano wa kimantiki na unategemewa kusababishwa na tokeo (Wamitila, 2006), mara nyingi inatarajiwa kuwa tukio linaloonekana katika fasihi limesababishwa hii ni kaida iliyotumiwa na mhakiki (Forster, 1927) katika kigezo cha kuelezea msuko. Majina mengi ya mitaa yameundwa kutokana na matukio ya kijamii yaliyotokea zamani. Majina yanayoteuliwa, huibua fikra au hisia fulani kuhusu masuala ya kijamii (Wamitila, 2004).

Jedwali Na 4.8: Mbinu ya Usababishi na Tukio

Na	Majina ya Mitaa	Shehia	Uhusiano
1.	Kisiwa ndui	Kikwajuni	Hii ni sehemu ya Kisiwa iliyotumika kuwekwa wagonjwa wa ndui
2.	Kibanda maiti	Nyerere	Palikuwa na kibanda cha kuoshea maiti
3.	Mlandege	Mlandege	Palikuwapo mtu akitega ndege na kuwala
4.	Rahaleo	Rahaleo	Majengo ya kisasa
5.	Shaurimoyo	Shauri moyo	Kuwapo wakaazi wenye tabia mbaya waliohimizwa kujishauri kwa ajili ya kujirekebisha.

Chanzo: Mtafiti (2014)

Mitindo ya kuundia majina inaonesha kuwa majina ya mitaa hayakuibuka tu bali kuna kaida maalumu zilizotumika kuundia majina hayo. Kaida hizo zimesaidia sana kutunza, kuhifadhi na kudumisha historia ya watu wa Unguja. Lyons (1971), alisema, muundo wa lugha, kifonolojia, kisarufi na kisemantiki, huelekezwa na kazi ambazo hufanywa katika jamii.

4.3.2 Lugha

Haji na wenzake (1981), Fasihi ni sanaa inayotumia lugha katika kuyasawiri mazingira pamoja na kuibua ufanisi katika maisha ya mwanadamu. Lugha ni kiini au uti wa mgongo wa fasihi, kwa sababu ndicho chombo cha kuiundia hiyo fasihi yenyewe. Lugha hutumika kwa mawasiliano, kati ya fanani na hadhira, ni chombo cha kuibulia hisia za hadhira.

Lugha ya kifasihi ni lugha teule iliyoteuliwa kwa madhumuni ya kuunda sanaa itayomvuta msikilizaji kwa mvuto wenye kunasa na kuathiri nafsi na hisia za hadhira. Lugha huchukua maumbo katika kazi ya fasihi. Miongoni mwa maumbo hayo ni: tamathali za usemi, mafumbo, tanakali sauti, takriri na udogoshi.

4.3.2.1 Tamathali za Semi

Mulokozi na Kahigi (1979), Tamathali za usemi ni vifananishi vya dhana fulani kwa dhana tafauti au mifanano. Ni usemi wenye kupanua, kupuuza au kubadilisha maana iliyokusudiwa na mtunzi. Tamathali za semi hutumiwa na wanafasihi ili kutia nguvu katika maana, kufanya kazi ivutie, kuipamba na kuongeza athari iliyokusudiwa. Tamathali za semi zilizotumika katika kazi hii ni tash biha, tauria. Sitiari na tash hisi.

Tash biha

Tash biha ni tamathali ya semi inayotumika kulinganisha vitu viwili kwa kutumia viunganishi kama vile; kama, mithili mfano na ja (wamitila, 2003). Mtaa unaoitwa, *Jang'ombe* umepewa jina hilo kutokana na ufananishi wa tabia za watu wake na tabia za ng'ombe, kwasababu ya kupenda vurugu na fujo kwa kutumia kiunganishi . “Ja” yenye maana kama ng'ombe.

Sitiari

Ni aina ya tamathali ya semi ambayo hujengwa kwa kufananishwa na kitu kingine bila ya kutumia kiunganishi.

Mitaa yenye umbo la sitiari:

Kaburi kikombe: Ni mtaa uliyolinganishwa na kaburi, kuwa kama kikombe

Begamoja: Ni jina linalofananisha umbali wa masafa ya bega moja tu kwa ukaribu.

Tauria/ Tafsida

Hii ni tamathali ya usemi ambayo hutumia maneno fulani kwa madhumuni ya kuziba karaha, uchafu na matusi ili kuwezesha, hata matusi, kutamkwa hadharani. Kunga hii ya usemi ikitumika katika fasihi, hujenga itifaki nzuri kwa watu katika mazungumzo yao ya kila siku (MULIKA, 1999). Mitaa iliyobeba sifa hii ni:

Mwembemchomeke: limepata jina hili kutokana na vitendo vya ubakaji vilivyofanyika pahali hapo huko nyuma.

Mchambawima: Kuchamba ni kujisafisha sehemu za siri kwa kutumia maji. (BAKIZA, 2010) Hii ni sehemu iliyokuwa na maji mengi. Watu walipopita walikunja nguo zao. Ndipo, ukazuka utani wa kupaita kwa jina hilo la Mchambawima.

Tash hisi

Hii ni tamathali ya usemi inayotumia mbinu ya kukipa kitu uhai au sifa ya kibinadamu, vitu ambavyo havina sifa hiyo (Greyson na wenzake, 2008).

Kibanda maiti: Mtaa huu umepata jina lake kwa kibanda kupawa
sifa ya umauti ambayo ni ya mwanadamu.

Mwembemimba: jina lake limetolewa kutokana na mwembe kupewa
sifa ya ujauzito, ambayo ni sifa ya mwanadamu, tena
awe mwanamke mzazi.

Mferejimaringo: Huu ni mtaa uliyopawa sifa ya maringo ambayo
ni sifa ya binadamu.

Kisiwandui: Ni mtaa uliopewa sifa ya kuwa na ndui, kwa kawaida
ndui ni ugonjwa anaopata binadamu.

Mtopepo: Ni mtaa uliyohusishwa na pepo
(shetani), kiumbe ambaye huingia ndani ya kiwiliwili
cha mwanadamu na kumchagiza.

Mkungumalofa: Ni mtaa uliyopawa ila ya ulofa ambayo ni hali inayompata
binadamu. Lofa ni mtu asiye na kazi, mzururaji au
ombaomba (BAKIZA, 2010).

Mafumbo

Wamitila (2003), Fumbo ni kauli ambayo huficha maana au ujumbe. Fumbo hilo hufumbuliwa na msikizaji baada ya kutafakari.

Mitaa ya mafumbo ni kama vile:

Shauri moyo: *Kutokana na vituko vya mtaa huo, ilibidi kila anaehamia,
Huambiwa, aushauri moyo wake.*

Rahaleo: Ni sehemu ambayo ilikuwa katika hali duni, na baada ya muda yakapatikana maendeleo ambayo yaliwapumbaza watu wengi

Mpendae: Ilinasibishwa na mapenzi ya kweli ya ndoa kwa wakaazi wake

Kajificheni: Kutokana na majengo na chochoro nyingi zilizofanana ziliwafanya watu wanaopita katika mtaa huo kupotea njia

Ziwatuwe: Ni mtaa wenye mchanganyiko wa wakaazi wake na wenye ugomvi sana

Tanakali Sauti

Tanakali sauti ni tamathali ya usemi inayotumiwa kurejelea sauti inayoigiza jinsi kitu fulani kinavyotendeka.

Bububu: Jina la mtaa huu limeundwa kutokana na sauti ya “*bu bu bu*” kuigizwa sauti ya treni iliyokuwa ikipita maeneo hayo miaka mingi iliyopita.

Takriri

Takriri ni usemi unaojidhihirisha kwa kurudiarudia neno, silabi au sentensi (MULIKA, 1999). Mtaa wenye muundo wa takriri ni:

Bububu: Jina hili limeundwa kutokana na kurejewa kwa silabi “*bu*”

Kwarara: Katika jina hilo kitu kinachojibainisha ni silabi iliyojirejelea, ambayo ni “*ra*”

Mwanakwerekwe: Jina hili limejirejea silabi “*kwe*”

Garagara: Jina lililoundwa kwa maneno mawili yaliyojirejea ambayo ni “*Gara na gara*”

Udogoshi

Udogoshi ni mbinu ya kukiita kitu kwa kukifanya kionekane kidogo. Mitaa yenye sifa ya udogoshi ni:

Kiembesamaki: Silabi “Ki” limetumika kudogosha mwembe.

Kinazini: *Pahala hapa pali hapo palikuwa na mnazi uliyodumaa, ulidogoshwa kwa silabi “ki” na kuitwa kinazini.*

Kikwajuni. Palikuwa na mkwaju mdogo hivyo pakadogoshwa na kuitwa kikwajuni

Kilima hewa: Ni mlima mdogo sana, nyumba zilizokuwa juu yake zilipata hewa safi pahala hapo palidogoshwa na kuitwa kilima hewa.

Lugha ya kifasihi huipa uhai na uhalisia zaidi dhana inayoelezwa, huburudisha na kuzindua akili ya msikilizaji au msomaji wa kazi ya fasihi na kuacha athari ya kudumu katika hisia na mawazo ya jamii. Majina ya mitaa iliyopo Mjini Unguja, yameundwa kwa kutumia ufundi mkubwa unaodhihirisha ufundi na ustadi mkubwa waliokuwa nao wazazi wetu wa kuitumia lugha yao ya Kiswahili inayowakilisha maisha halisi ya Mswahili, akiwa katika harakati zake za kimaisha na mazingira yaliyomzunguka.

Lugha iliyojaa utamu na ladha ya hali ya juu kabisa kwa yule aliye mweledi wa lugha hii, mwenye kuifahamu ndani nje, ndiye atakayeng’amua vionjo vilivyotumika katika majina hayo. Nadharia ya ndani nje imemuongoza mtafiti kuweza kugundua usanii na ufundi wa lugha iliyotumika katika majina ya mitaa.

4.4 Ujumbe wa Majina ya Mitaa

Haya ni madhumuni ya tatu ambayo mtafiti amechambua ujumbe unaopatikana katika majina ya mitaa kwa kuonesha ujumbe wa kijumla na ujumbe makhsusi wa kila jina.

Ujumbe ni dhanna inayotumiwa kuelezea taarifa ambayo msanii huitoa kwa wasomaji au hadhira kama njia moja ya kuhakiki kuwa dhamira. Mhilu na wenzake (2008), wamefafanua kuwa, ujumbe ni mafunzo ambayo msomaji au msikilizaji wa kazi ya fasihi anayapata baada ya kung'amua dhamira zilizojitokeza. Aghalabu, ujumbe hutumia lugha ya mkato yenye mafunzo ndani yake, yenye muundo wa msemo au methali. Majina yana dhima kubwa katika maisha ya jamii. Ujumbe unaopatikana ndani ya majina ya mitaa unaakisi hali halisi ya maisha ya watu wa Unguja. Majina yana dhima ya kuonesha utamaduni, utambulishi na uhifadhi wa historia ya jamii.

4.4.1 Utamaduni

Lugha ni kielezeo kikubwa cha utamaduni wa jamii. Bukenya (1994) amesema kuwa, fasihi ni sehemu ya masimulizi ya utamaduni wa jamii. Kuna uhusiano wa moja kwa moja, kati ya majina ya mitaa na harakati za kimaisha za jamii. Majina ya mitaa yamesheheni utamaduni halisi wa watu wa Unguja. Yapo majina kama vile *Kundemba*, *Mwembebeni*, *Mwembematarumbeta* yanayowakilisha sanaa ya burudani na sherehe za kizanzibari. *Mwembeladu*, *Migombani*, *Mshelishelini*, *Mwembenjugu* yanaelezea utamaduni wa vyakula. *Kibandamaiti*, *Kaburikikombe*, *Kijitoupele*, *Mtopepo* na *Makadara* inathibitisha imani na itikadi waliyonayo wanajamii kuhusu mambo ya kiroho kamavile kujiandaa kwa kifo, kuamini pepo na

mashetani, kujali tiba asilia na kukubaliana na maamuzi ya Mungu. Mwembetanga, Mwembemadema, Kiembesamaki inadhihirisha sanaa ya uvuvi katika maeneo ya pwani. Hivyo, kwa kupitia majina ya mitaa tunaweza kuona viashiria vya utamaduni katika jamii ya Unguja Mjini.

4.4.2 Utambulishi

Utambulishi una jumla ya vigezo maalumu vinavyotumika. Mtu, kundi la watu, jamii au taifa fulani huwa tafauti na taifa jengine, jamii fulani iko tafauti na jamii nyengine au mtu fulani yuko tafauti na mwengine, mtaa nao uko tafauti na mtaa mwengine (Msanjila na wenzake, 2009). Majina ya mitaa hutolewa kwa lugha inayoeleweka na wanajamii, iliyobeba maana inayotokana na utamaduni wa mazingira na kuitambulisha jamii. Kwa mfano, mtu anaposema, mimi ninaishi mtaa wa *Mbweni*.

Msikilizaji anaweza kupata ujumbe kuwa, mtu huyo ni mwenye cheo, tajiri au ana hadhi kubwa. Vilevile mwengine akisema mimi ninaishi *Mkungumalofa*, basi itafahamika kuwa, ni masikini hawezi hata kupata kula yake. Majina ya mitaa, hutambulisha koo za watu. Mtu anaposema, mimi ninatoka *Tumbatu*, itafahamika kuwa huyu ni Mtumbatu, dini yake fulani na chakula chake kadhaa.

Utambulishi husaidia watu kuthamini tamaduni zao. Kumekuwa na wimbi la vijana, kuanzisha maskani na kuzinasibisha na majina ya Ulaya. huo ni unyonge mkubwa. Waswahili wanasema “Mkataa kwao mtumwa” Iwapo jamii itakataa majina yao ya asili, watauza thamani yao ya utambulishi kwa bei hasi. Jamii inapothamini utambulishi wao huwa na nguvu kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

4.4.3 Kuhifadhi Mapisi

Hoopes (1979) anasema kuwa, masimulizi ya kimapisi yanatokana na mazungumzo ya mtu binafsi juu ya maisha ya watu wanaomzunguka na matukio yanayotokea. Kila jamii ina mapisi ya maisha yake. Majina, kama vile, *Kisiwandui*, ni kumbukumbu ya maradhi hatari ya ndui yaliyotokeza katika miaka ya (1880). *Darajani* inatoa kumbukumbu ya mazingira ya bahari iliyokuwapo katika eneo hilo. Ni vigumu kwa mtu wa kisasa, kufahamu kwamba pahala hapo, palikuwa ni mkondo wa bahari. Jina la *Darajani* litaendelea kuhifadhi kumbukumbu hiyo. *Kibandamaiti*, ni sehemu iliyokuwa ikitumika kuoshea maiti.

TUKI (2003) wamemnukuu Mw. Nyerere, akisema kuwa “jifunzeni kwa wazee wenu na babu zenu, hadithi, mashairi na historia ya watu wenu maana mambo hayo hayaandikwa vitabuni, hivyo, ni lazima muyajue na muyafundishe kwa wengine. Jamii bila ya kumbukumbu ni sawa na gari bila usukani. Mbali ya ujumbe wa jumla, majina ya mitaa, yanatoa ujumbe mahsusi kwa jina, kama jina pekee, kama tunavyoona katika jadwali.

Jedwali Na 4.9: Ujumbe wa Majina ya Mitaa

Na	Mtaa	Ujumbe
1	<i>Kajificheni</i>	Kuwa na hadhari
2	<i>Pitanazako</i>	Kuepuka mambo ya watu
3	<i>Mpendae</i>	Mapenzi ya kweli yametawala
4	<i>Jang'ombe</i>	Mtu si ng'ombe
5	<i>Mwembemchomeke</i>	Hadhari dhidi ya vitendo viovu
6	<i>Mkungumalofa</i>	Ukata uliokithiri
7	<i>Mwembeshauri</i>	Mafanikio huja kwa kushauriana

8	<i>Makadara</i>	Mwenyezi Mungu Ndiye Mpangaji wa yote
9	<i>Rahaleo</i>	Maendeleo yamepatikana, ya jana si ya leo
10	<i>Kijitoupele</i>	Vitu vya asili ni tiba
11	<i>Kibanda maiti</i>	Tujiandae na kifo
12	<i>Shaurimoyo</i>	Fikiria kabla ya kutenda
13	<i>Muungano</i>	Umoja na Mshikamano ni jambo jema
14	<i>Mchambawima</i>	Sitara ni bora kuliko kujiumbua

Chanzo: Mtafiti (2014)

Nadharia ya ndani nje inalazimisha mtafiti, kabla ya kufanya utafiti au kutoa hitimisho la aina yoyote linalohusu jamii. Jambo la msingi kwake ni kuijua jamii hiyo ndani nje. Majina ya mitaa ya Unguja Mjini yanadhihirisha utamaduni wa watu wa Unguja, yamehifadhi historia yao nanikielelezo kizuri cha utambulishi, jambo ambalo ambalo mgeni hawezi kuligundua. Katika utafiti huu nadharia ya ndani nje ni muhimu sana katika kufikia hitimisho sahihi la utafiti kuhusu kuchunguza fasihi ya majina ya mitaa ya Mjini Unguja.

4.5 Hitimishi

Kwa ujumla katika sura hii yameainishwa majina kwa kuyagawa katika makundi, yapo majina yaliyotokana na miti, watu, mazingira na majina ya matukio. Vilevile imechambuliwa fani iliyounda majina hayo kwa kuangaliwa kipengele cha mtindo na lugha, imeelezwa asili ya majina na ujumbe unaopatikana katika majina ya mitaa.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHI NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza fasihi ya majina ya mitaa ya Mjini Unguja. Data zilikusanywa kutoka katika mitaa ya Jang'ombe, Rahaleo na Mji Mkongwe. Mtafiti alitafiti fasihi ya majina kutoka kwa watafitiwa ambao walionekana kuijuwa vyema fasihi ya majina. Baada ya kukusanya, mtafiti alichambua data alizozipata kwa njia ya maelezo kwa kuongozwa na nadharia.

5.2 Muhtasari

Utafiti huu umegawika katika sura tano ambazo zimechunguza fasihi ya majina ya mitaa. Katika sura ya kwanza mtafiti aliweza kubainisha vitu muhimu vya utafiti, kwanza, mtafiti alielezea usuli wa mada, ambapo mtafiti alielezea kwa ufupi dhanna ya majina kwa kufafanua fasili ya majina, umuhimu na mapisi ya majina katika maisha ya mwanadamu. Pia mtafiti hakuacha kuelezea tatizo la utafiti kwa kuchambua fasihi ya majina. Jina kama uwa lililofumba lenye mambo mengi ndani yake, linalohitaji ujuzi kulifumbua. Chimbuko la tatizo hilo limesababisha kuibuka kwa majina mengi mapya yasilandana na utamaduni na utambulishi. Lengo kuu la utafiti ni kuchunguza fasihi ya majina ya mitaa. Lililoambatana na madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake.

Katika sura ya pili, mtafiti alitalii tasnifu, wavupepe magazetini na vyombo vya habari ili kupata maelezo yaliyohusiana na mada. Mtafiti aligundua kuwa tafiti na kazi nyingi kuhusu majina zimejadiliwa katika mkabala wa isimu jamii zilizoelezea

asili ya majina na njia za kuundia majina, ingawa mada kuhusu fasihi ya majina bado haijashuhulikiwa ipasavyo. Kazi tangulizi zilizopitiwa ni zile zinazohusu asili ya vitu, koo na majina ya semi, maandishi yanayohusu asili ya majina yalisaidia kubaini njia zinazotumika kuundia majina.

Kwa upande mwingine, yaliyohusu semi yalisaidia kugundua mbinu ya kuhakiki kifasihi zilizotumika kuchambua, semi za daladala, tiketi za bajaji na semi za mafumbo ya kanga zilichambuliwa kifani na kimaudhui. Hata hivyo, marejeleo yote yaliyopitiwa yalimsaidia mtafiti katika kubainisha pengo na kumsaidia kusukuma mbele utafiti kwa kuweka wazi fasihi iliyomo ndani ya majina.

Aidha, kiunzi cha nadharia kilichojadiliwa kuongoza na kubainisha utafiti huu ni nadharia mbili ambazo ziliongoza utafiti, nadharia mama ilikuwa nadharia ya ndani nje ambayo imeshiriki kuchukua nafasi katika malengo mawili ya utafiti ambayo ni kuchunguza mtindo, lugha na ujumbe. Hata hivyo, nadharia ya uhalisia iliongoza lengo la kwanza la kuchunguza asili ya majina ya mitaa.

Sura ya tatu mtafiti alibainisha mbinu na njia za utafiti alizozitumia katika kukamilisha utafiti, hapa mtafiti anaandaa utaratibu mzima wa kufanya utafiti kuanzia mwanzo hadi mwisho, uteuzi wa njia bora ni muhimu katika utafiti. Katika utafiti huu mtafiti alitumia njia ya usaili na hojaji, kama kawaida hakuna kizuri kisicho kasoro. Matatizo ya ucheleweshaji wa hojaji na nenda rudi yalitawala katika utafiti. Hata hivyo, wasaidizi wa mtafiti walitumika ipasavyo, walishirikiana naye mkono kwa mkono hadi kukamilika kwa utafiti huu.

Sura ya nne, ilihusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti. Majina ya mitaa sabini na tano yalikusanywa na kuwekwa katika makundi yafuatayo; Majina yaliyotokana na miti, majina ya watu, majina ya mazingira na majina ya matukio ya kihistoria. Mtafiti alichambua asili ya majina ambapo mtafiti alielezea sababu zilizopelekea mitaa hiyo kupewa majina hayo kwa kuchambua maelezo ya watafitiwa, alichunguza fani katika kipengele cha mtindo na lugha na mwisho, kueleza ujumbe unaopatikana katika majina kwa kuchambua ujumbe wa jumla wa majina kama vile kulinda utamaduni, utambulishi na kuhifadhi historia. Mwisho ni sura ya tano ambayo ilitoa muhtasari, matokeo ya utafiti yalibainishwa na mapendekezo ya utafiti yalitolewa kwa serikali, wanajamii na watafiti wa sanaa jadiya.

5.3 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kukusanya na kuchanganua data, kuhakiki na kueleza fasihi ya majina ya mitaa. Kwavile fasihi ni kioo cha jamii huimurika kila sehemu inayoelekezewa. Fasihi ya majina bila ya kuwa na darubini iliyokomaa huwezi kuiona, lazima uwe mweledi wa kuifahamu fasihi ndani nje. Kazi hii imetudhihirishia kuwa majina ya mitaa yana ufundi wa kifasihi. Mtafiti ameutudhihirisha ufundi huo kwa kuchambua vipengele vya fani na maudhui.

Utafiti huu ulikuwa na madhumuni matatu, ambayo ni kuchunguza asili ya majina, kuchambu kipengele cha mtindo na lugha na mwisho kutoa ujumbe wa majina ya mitaa. Mtafiti aliyatumia madhumuni hayo kama dira ya kufikia hitimishi lake. Matokeo yanaonesha kuwa, majina ya mitaa yameundwa kwa kutumia lugha ya kifasihi yenye mvuto, inayotoa taswira kwa jamii. Zimetumika tamathali za semi

kama vile tash biha, tauria, tash hisi, mafumbo na tanakali sauti. Kazi hii inadhihirisha kuwa majina ya mitaa yameundwa kwa kutukia mbinu ya mwambatano, mbinu ya kuhusisha na mazingira (toponimu), mbinu yakuhusishwa na mtu mashuhuri (eponimu) na mbinu ya usababishi. Yote hayo, yanaonesha fasihi iliyomo ndani ya majina ya mitaa ila hawezi kuiona isipokuwa anayejuwa fasihi ya jamii ndani nje.

Mtafiti alichunguza asilli ya majina na kugundua kuwa, majina hayo yameanza kwa sababu maalumu za kihistoria na kimazingira. Watafitiwa wote walikiri kuwapo kwa asili, majina yalianza kutokana na matukio muhimu yaliyotokea, jamii inapaswa kufahamu mapisi yao. Watu wengi, hasa vijana, hawajui umuhimu wa mapisi yao na utamaduni wao, hali hii imesababisha kuiga utamaduni wa kigeni unaobomoa utambulishi wetu. Fasihi ina kwao, kila jamii ina fasihi yake, iliyoshikamana na silka, mila na utamaduni. Kuna mitaa mingi iliyopawa majina ya kigeni, wazee wameonesha wasiwasi wao kuhusu kupotea kwa utamaduni na utambulishi wa asili ingawa wengine walisema fasihi inakwenda na wakati.

Hivyo, matokeo ya kazi hii yatakuwa chachu kwa wanasanaajadiya kuendelea na kuhifadhi utamaduni, utambulishi na historia ‘Mtu kwao na watu na vyao’ ndiyo ngao ya kuishikilia ili kizazi kijacho kisizame ndani ya dimbwi la ukoloni mamboleo.

Kipya ambacho mtafiti amekigundua katika utafiti, kuna baadhi ya majina yameundwa kwa kudondosha baadhi ya sauti au maneno, mfano, Kwamtipura, mwanzoni kukiitwa Kwa mtip tip. Ziwatuwe, kukiitwa Ziwatuwe roho zao. Pia,

baadhi ya majina ya mitaa sasa hayatumiki tena, majina kama vile Mtakuja, Rahakesho, Mwembeboso, Mianzini na Kachorora. Vile vile utafiti umeonesha kuwa majina mengi ya mitaa iliyopo Mjini Unguja inatokana na miti, milima, na hali nyengine za kimazingira kutokana na watu kuelewa zaidi mazingira yao yaliyowazunguka.

5.3 Mapendekezo

Kwa kawaida matokeo ya utafiti ni kama darubini ya kuona mbele na kutafakari cha kufanya katika nyanja ya kitaalimi, utafiti huu ni chembe ya sukari ndani ya bahari. Elimu ina kwao na fasihi ina kwao, kwa hali hiyo Wanataalimu, wanazuoni na wanafunzi wa ndaki katika sanaajadiiwa wajitowe kimasomaso katika kuhamasisha, kuandika na kufanya tafiti zaidi juu ya mada hii ndani ya eneo la utafiti na nje ya eneo, kwani majina ni dhana muhimu sana kwa upana wake iliyochelewa kufanyiwa tafiti.

Licha ya kuchunguzwa fasihi ya majina katika vipengele vya lugha, mtindo na ujumbe, bado kuna pengo la kuchunguza vipengele vyengine vya kifasihi kama vile muundo, mitindo mingine ya lugha, maadili yanayopatikana ndani ya majina na mbinu nyenginezo za kisanaa. Pia, wanataalimu wa sanaajadiiwa wachunguze na kuandika utanzu huu wa majina kama zilivyo tanzu nyengine za nahau na methali.

Ili kufanikisha utafiti, lazima ndani ya kila Wilaya, kila Maktaba kuu ya Nchi na ndaki, kwenye Hifadhi maalumu na makumbusho ya Taifa kuwe na maktaba maalumu za utafiti, buku la watafiti wajaji, rekodi zote na vitabu maridhawa vya

wabobezi wa utafiti, tasnifu za ndani na nje ziweze kupatikana na kuhifadhiwa kwa ajili ya kurahisisha kazi za utafiti nchini. Pia, ili utafiti ukidhi haja za jamii, miundo mbinu na huduma za kijamii lazima ziimarishwe.

Mtafiti anaamini kuwa kazi hii itakuwa mwanzo mpya na mzuri wa kuthamini lugha adhimu ya Kiswahili kwa kuwa imekidhi nia ya kufanya utafiti huu wa kuchunguza fasihi ya majina ya mitaa ya Mjini Unguja.

MAREJELEO

- Abeid, B. (2005). Makala ya Bakari Abeid. *Makala ya Kiswahili Zanzibar*.
(haijachapishwa).
- Abubakar, A.M. (1998). *Zanzibar Hapo Kale*. Zanzibar: Masomo Book Shop.
- Al Farsi, A. S. (1993). *Kur ani Takatifu*. Nairobi: The Islamic Foundation.
- Alhidaaya. (2015). *Majina ya Watoto*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Ally, J. na Mustafa, H. (1930). *Nahau-Al-Waadhih. Daaru Maarifa*: Misri, Oxford University Press.
- Amiri, H. J. (2011). Matumizi ya Majina Katika Utambulishi wa Jamii ya Watanzania: M.A. Kiswahili Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Tanzania.
- Bakhressa, S. K. (1999). *Kamusi ya Maana na Matumizi*. Nairobi: Oxford University Press.
- BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.
- BAKIZA, (2011). *Makala za Kisemina ya Kumuenzi Mwandishi Muhammed Said Abdullah*: Zanzibar: Baraza la Kiswahili Zanzibar.
- Bell, C. (1806). *Essays on the Anatomy of Expression in Painting*. London: Routledge.
- Bubenya, A. (1994). *Understanding Oral Literature*. Nairobi: Nairobi University Press.
- Buberwa, A. (2010). Investigating Sociolinguistic Aspects of place in Ruhaya in North-West Tanzania. (M.A Dissertation). University of Dar es Salaam, Tanzania.

- Buberwa, A. (2010). *Muundo wa Majina ya Mahali Katika Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Majina ya Vituo vya Daladala Jijini Dar es Salaam*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.
- Buberwa, A. (2011). *Muundo wa Majina ya Mahali Katika Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Chande, M. O. (2014). *Kuchunguza Dhima ya Mafumbo ya Kanga Katika Jamii ya Unguja Mjini*. M.A Kiswahili Chuo Kikuu Huria Cha Dar es Salaam, Tanzania.
- Chomboz. BlogSpot. Com /p/ 18/11/2014, Bubujiko la Maarifa 6:32 p.m
- Chum, H. (1982). *Desturi na Mila Zetu*. East Africa Publication Limited Arusha.
- Cohen, L. na Keitle, M. (2001). *Research Methodology Education*. London: Routledge Farmer.
- Dekeba, A. (2012). Basics of Marketic Research Methods Retrieved on 11th May, 2016 from: [www.globusz. Com /ebook/Marketing Research/ Index.htm](http://www.globusz.com/ebook/Marketing%20Research/Index.htm).
- Denice, S. (2011). *Haja ya Kuundwa Kamusi ya Majina ya watu ya Asili Katika Jamii ya Wahaya*: Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Denscombo, M. (2005). *The Good Research Guide for Small Scale Social Research Project*. New York: Open University Press.
- Denscombo, M. (2005). *The Good Research Guide for Small Scale Social Research Project*, New York, Open University Press.
- Dosha, A. (2010). *Mchango wa Hadithi Katika kuendeleza Jadi*, Mila za Waha Kata ya Mububo na Wilaya ya Kasulu. M.A. Kiswahili: Chuo Kikuu Huria Dar es Salaam, Tanzania.

- Enon, J. C. (1998). *Educational Research Statistic and Measurement*. Kampala
Department of Distance Learning: Kampala: Makerere University.
- Forster, E. M. (1927). *Aspects of the Novel*. London: Penguin Books.
- Franta, H. na Althoen, S., (1994). *Statistics Concepts and Application*. New York:
Cambridge Universty Press.
- Gichuru, T. M. (2010). Uchanganuzi wa Nomino Ambatano za Kiswahili: Mtazamo
wa Mofolojia Leksia Tasnifu ya Umahiri (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha
Kenyatta. Nairobi, Kenya.
- Haji, A. Hamad, A. na Omar, M. (1981). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. Zanzibar:
TAKILUKI
- Haji, M. O. (2013). Nafasi ya Hadithi Simulizi Katika Kufunza Maadili Mema Shule
za Sekondari, Visiwani Zanzibar. (Phd. Kiswahili). Chuo Kikuu Huria Cha
Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.
- Haji, M. U. na Rai, C. (2009). Dhima ya Michenzo ya Watoto ya Jadi Katika Jamii
ya Wamakunduchi. (Haijachapishwa), Zanzibar, Tanzania.
- Haji. M. Kh (2014). Uchanganuzi wa Kiisimujamii ya Mifumo ya Utoaji wa Majina
ya Mitaa Katika Mkoa wa Kusini Unguja. M.A Kiswahili Chuo Kikuu Cha
Kiislamu Uganda. Kampala, Uganda.
- Hassan, N. (2010). *Mitindo naMatumizi ya Lugha Utafiti Katika Semi za Bajaji*. Dar
es Salaam: Chuo Kikuu Cha Dares Salaam.
- Hoopes, J. (1979). *Oral History An Introduction for Student*. Carolina: The
University of North Carolina, Chapel Hill.
- Ingram, W. H. (2007). *Zanzibar its History and Its Peoples*. London: Stac of
International.

- Juma, M. A. (2011). *Mfanano wa Lahaja za Kimakunduchi, Kibwejuu na Kizimkazi*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.
- Kennan, P. M. (2007). *Narrative Fiction*. London: Raitledge.
- Khamis A. A. (2011). *Uchambuzi wa Kiswahili Fasaha*. Zanzibar: Chuo Kikuu cha Elimu Chukwani Zanzibar.
- Khamis, K. S. na Omar, H. H. (1993). *Historia Fupi ya Zanzibar* Chapa ya Kwanza Idara ya Nyaraka na Makumbusho ya Kale Zanzibar.
- Kihore, Y. M. na Chuwa, M. (1999). *Kiswahili Katika Karne ya Ishirini na Moja*: Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Kihore, Y. M. (2009). *Isimu Jamii Sekondari na Vyuo*: Chuo Kikuu Dar es Salaam. TUKI.
- Kivenule, A. (2013). *Chimubo – Na Historia – Ya – Uhehe* – Html Blog Spot .Com.
- Kothari, C.R (2009). *Research Methodology. Method and Techniques*, Second Revised Edition, New Delhi: New Age International (P) Ltd.
- Lyons, J. (1971). *An Introduction to Theoretical Linguistics*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Masebo, V. (2010). *Kiswahili kwa Shule za Kiswahili, Kidato cha Tatu na Nne*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.
- Masoud, F. A. (2005). *Nafasi ya Visasili Katika Jamii ya Leo ya Zanzibar*.Tasnifu ndogo. Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar. Zanzibar: SUZA.
- Massamba, D. (2014). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*, SAMIKISA Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

- Massamba, D.P. na Kihore, Y.M (2012). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu. Sekondari na Vyuo. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*
- Mbijima, R.J (2011). *Dhima ya Visasili Katika Jamii ya Wagogo: M.A. Kiswahili: Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.*
- Mdee, J.SnaMasaba (2002). *Mulika Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. M.A. Kiswahili. Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.*
- Mhilu, C. na Wenzake (2008). *Tahakiki Vitabu Teule vya Fasihi 3 4 Kidato cha Nne Nadharia, Uhakiki na Mswali. Nyambari Nyangwine Publisher.*
- Mlacha. S. na Hurkeinein (1995). *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili: Dar es Salaam.*
- Moh'd, M. N. (2009). *Uchanganuzi wa Taashira za Kauli Zilizandikwa Katika Gari za Abiria Kisiwani Unguja. (M.A. Kiswahili). Chuo Kikuu Cha Kiislamu: Uganda*
- Mrikaria, G. (2004). *Katagoria za Kisarufi Katika Uundaji wa maneno. Mradi wa Kiswahili Program Huria, Warsha ya Arusha Novemba 1/5 Arusha Tanzania.*
- Msanjila, Y.P .na Wenzake (2009). *Isimu Jamii, Sekondari na Vyuo. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dares Salaam.*
- Mtoro, N. G. (2011). *Tathnifu ya M.A. Kiswahili, Dhima ya Semi Zilizandikwa Katika Daladala. M.A. Kiswahili. Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.*
- Mulokozi M. M. (1990). *Fasihi ya Kiswahili: Chuo Kikuu Huria Dar es Salaam.*
- Mulokozi, M. M na Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.*
- Mussa, V. (1980). *Mkwava na Kabila Lake. Arusha: East African Bureau Arusha.*

- Mutembei, A. K. (2009), *UKIMWI Katika Fasihi ya Kiswahili* Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dares salaam.
- Mwalugaja, D. (2013). *Historia ya Wanyakyusa*. Dar es Salaam: Global Publishers
- Mwaruka, R. (1965). *Masimulizi ya Wazaramu*. London: Macmillarn Company Ltd.
- Ndalu, na Kungei, K. (2008). *Kamusi ya Methali*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Ndamba, J. A. (2012). *Kufuwawa kwa Miiko na Kupotoka kwa Maadili, Uchunguzi Kifani wa Jamii ya Wabungu. Shahada ya Uzamili Katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania*. Dar es Salaam, Tanzania.
- Ndumbaro, E. F. (2014). *Dhima na Dhamira katika nyimbo za Kabila la Wamatumbi*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili na Isimu
- Ndungo, M. na Mafula, R. (1991). *Nadharia ya Fasihi Simulizi* Nairobi: University of Nairobi.
- Oliver, P. (2004). *Writing Your Thesis. Second Edition*. London: Oliver's Yard.
- Opie. C. (2010). *Doing Education Research*. London: Rolivers's Yard.
- Pons, V. (1992). *Introduction to Social Research*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Prewitt, K. (1990). *Introductory Research, Methodology, East African. Applications Occas, Oral Papers no; 10*. Institute of Development Studies, University of Nairobi. Kenya.
- Rashid, H. U. (2011). *Mafunzo ya Nyimbo za Jando na Unyago kwa Jamii ya Wahiyao wa Masasi*. M.A. Kiswahili Chuo Kikuu Huria Tanzania.
- Redio nour, (2013). *Kipindi cha Tutunze Historia Yetu*. Redio Nour Zanzibar.

- Saleh, T. (2011), *Dhima ya Nyimbo Katika Matambiko ya Wazaramu*. (M.A. Kiswahili): Chuo Kikuu Cha Dares salaam. Tanzania.
- Saluhiya. M. C. (2010). *Kiswahili-1, Nadharia ya Lugha Kidato Cha Tano na Sita*. Children. Dar es Salaam: Education Society.
- Seif, D. G. (2011). *Nyimbo za Jando Katika Jamii ya Kikagur, Kata ya Gairo*. M.A.Kiswahili Morogoro Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Morogoro, Tanzania.
- Sengo, T. S. Y. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: Al-amin Education and Research Academy.
- Sevenye, W. na Robinsonm, R. (2001). *Qualitative Reaserch Issue and Methods*. New Youk: Art Introduction for Education Technologist.
- Simiyu, F. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi Kwa Shule, Vyuo na Ndaki*. Dar es Salaam: Serengeti Bookshop.
- Strictly, G. (2010). *Fahamu – asili – na – maana ya jina lako*HH; Dar esSalaam: Word Press.Com.
- Taboretu, K.A. (1989). Seminar D’anth ropologic du Languge, MSH-Information, *Bulletin de la Fondation des Sciences de l’Homme*,5(9), 15-17.
- TUKI, (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Dar es Salaam: Oxford University Press.
- TUKI, (2003). *Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili.111 Fasihi*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Toleo la Pili*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Dar es Salaam: Oxford University Press

TUKI, (1999). MULIKA.Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Verschuren, P. and Doorewaard, H. (2005). LEMMA Nertherlands.

Wamitila, K.W (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi, Nairobi*: English Press.

Wamitila. K W. (2006). *Uhakiki waFasihi, Misingi na Vipengele Vyake*: Nairobi Kenya limited.

Wamitila. K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istillah na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Ltd.

VIAMBATANISHI

Kiambatanishi Na. I: Maswali ya Usaili kwa Wazee

1. Jina lako Jinsia
- Umri wako Tarehe
- Unapoishi.....Kazi.....
- (a) Taja mitaa mingine mitatu ya Mjini unayoifahamu
 - (i) (ii)
 - (iii)

2. Taja mitaa miwili na asili ya jina lake
 - (i) Mtaa.....
 - Asili yake
 -
 -
 - (ii) Mtaa
 - Asili yake
 -
 -
 -

- 3 Kwa kawaida majina mengi ya mitaa yana asili mfano;

Michenzani, asiliyake ni mtaa ambao ulikuwa na michenza mingi

Toa asili ya mitaa ifuatayo:

- (i) Kaburikikombe.....
.....
- (ii) Darajabovu.....
.....
.....
- (iii) Kilimahewa
.....
.....
.....
- (iv) Ziwatuwe
.....
.....
.....

4. Baadhi ya Majina ya mitaa yana muundo wa kigeni. Mfano:
Jina Toronto, Kutoka Nchini Canada
Nyarugusu, kutoka Tanzania Bara

Toa jina la mtaa wenye asili ya kigeni

- (i) Jina.....
(ii) Kutoka

5. Majina hujitokeza katika asili yake kutokana na vipengele kama; Mimea, Watu, Wanyama, Mazingira na Matukio. Taja mitaa inayotokana na asili zilizotajwa.

Asili ya Mimea	Asili ya Watu	Asili ya Wanyama	Asili ya Mazingira	Asili ya Matukio
Mikunguni	K/ Haji tumbo	Kichaka Punda	Kilima hewa	Kibanda Maiti
1.				
2.				

6. Majina ya mitaa hutolewa kwa kuzingatia kigezo gani katika jamii ya Unguja?

Chagua jawabu sahihi kwa kuweka alama ya {v}

- (i) Asili ya pahali { }
- (ii) Huzuka kutokana na tukio { }
- (iii) Kutoa ujumbe { }
- (iv) Mapenzi ya mtu binafsi { }
- (v) Yote { }

7. Majina yafuatayo yanatoa ujumbe gani?

Kajificheni:

Kisiwandui:

Shaurimoyo:

8. Toa ushauri kitu gani kifanyike ili kutunza na kuenzi majina ya asili ya mitaa?

.....

.....

.....

.....

AHSANTE SANA

Kiambatanishi Na. II: Maswali ya Hojaji kwa Viongozi

1. Jina lako Jinsia

Umri wako Tarehe

UnapoishiKazi.....

(a) Taja mitaa mingine mitatu ya Mjini unayoifahamu

(i) (ii)

(iii)

2. Taja mitaa miwili na asili ya jina lake

(b) Mtaa.....

Asili yake

.....

.....

.....

(b) Mtaa

Asili yake

.....

.....

.....

(c) Kwa kawaida majina mengi ya mitaa yana asili mfano;

Michenzani, asiliyake ni mtaa ambao ulikuwa na michenza mingi

Toa asili ya mitaa ifuatayo:

(v) **Kaburi kikombe**.....

.....

- (vi) **Daraja bovu**.....

- (vii) **Kilima hewa**

- (viii) **Ziwa tuwe**

4. Baadhi ya Majina ya mitaa yana muundo wa kigeni. Mfano:

Jina **Toronto**, Kutoka **Nchini Canada**

Nyarugusu, kutoka **Tanzania Bara**

Toa jina la mtaa wenye asili ya kigeni

Jina.....Kutoka

5. Majina hujitokeza katika asili yake kutokana navipengele kama; Mimea, Watu, Wanyama, Mazingira na Matukio. Taja mitaa inayotokana na asili zilizotajwa.

Asili ya Mimea	Asili ya Watu	Asili ya Wanyama	Asili ya Mazingira	Asili ya Matukio
Mikunguni	K/ Haji tumbo	Kichaka Punda	Kilima hewa	Kibanda Maiti
1.				
2.				

6. Majina ya mitaa hutolewa kwa kuzingatia kigezo gani katika jamii ya Unguja?

Chagua jawabu sahihi kwa kuweka alama ya { v }

Asili ya pahali { }

Huzuka kutokana na tukio { }

Kutoa ujumbe { }

Mapenzi ya mtu binafsi { }

Yote { }

7. Majina yafuatayo yanatoa ujumbe gani?

Kajificheni:

Kisiwandui:

Shaurimoyo:

8. Toa ushauri kitu gani kifanyike ili kutunza na kuenzi majina ya asili ya mitaa?

.....

.....

.....

.....

AHSANTE SANA

Kiambatanishi Na. III: Majina ya Mitaa**Majina ya Mitaa Yenye Asili ya Miti**

1. Mwembeladu
2. Mwembeshauri
3. Mwembebeni
4. Mwembekisonge
5. Mwemberikunda
6. Mwembetanga
7. Mwembeshauri
8. Mwembemadema
9. Mwembemakumbi
10. Mwembemimba
11. Mwembedezo
12. Mwembemchomeke
13. Mwembematarumbeta
14. Miembeni
15. Kiembesamaki
16. Mbuyupacha
17. Mbuyutaifa
18. Mbuyukidambwita
19. Mbuyumnene
20. Mbuyu
21. Migombani
22. Mkunazini
23. Mikunguni
24. Mshelishelini
25. Misufini
26. Mkungumalofa
27. Michenzani
28. Mtendeni
29. Mkamasini
30. Kinazini
31. Mlandege
32. Kikwajuni

Majina ya Mitaa yenye Asili ya Watu

1. Kwahani
2. Kwaalinatoo
3. Kwaalimsha
4. Kwahajitumbo
5. Kwamtipura
6. Kwabiziredi
7. Kwasharifumsa
8. Amani
9. Lumumba
10. Nyerere

Majina yaliyotokana na Mazingira

1. Kidongochekundu
2. Kidutani
3. Kilimahewa
4. Kilimani
5. Kijangwani
6. Mtoni
7. Mchangani
8. Vikokotoni
9. Darajani
- 10 Kijitoupele

Majina ya Mitaa Yanayotokana na Matukio

1. Kisiwandui
2. Kibandamaiti
3. Rahaleo
4. Kajificheni
5. Mchambawima
6. Shaurimoyo
7. Mpendae
8. Muungano
9. Begamoja
10. Bububu

11. Gulioni
12. Makadara
13. Ziwatuwe
14. Kindemba
15. Magomeni
16. Kariakoo
17. Jang'ombe
18. Kaburikikombe
19. Mferejimaringo
20. Mwanakwerekwe
21. Saateni
22. Muungano